# Nipashe

Jumanne Desemba 12, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0581522

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




**CASEMIRO AIPA MATUMAINI MAN UNITED**

UKURASA 22



TIBA YA FIGO

# Rais Samia kumsaidia Profesa J

• **Afika** ukumbini akisukumwa kwenye kiti mwendo; Lissu, Mnyika wasema... *Ukurasa 2*

UKURASA WA 5

**Makamu** wa Rais Zanzibar apigia chapuo Kiswahili kimataifa

UKURASA WA 19


**Ikibaki** wiki, vifaa uchaguzi DRC vyatua toka China

UKURASA WA 19

**Israel** yahamia wito UN ipeleke misaada Gaza

## Nape atangaza msako wazushi kifo cha Mpango

UKURASA 2



Soko la Samaki Kakukuru, wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza likiwa limebomolewa na maji yanayosogea ya Ziwa Victoria.
PICHA: SANULA ATHANAS

RIPOTI MAALUM

# Makazi, mashamba ya kisiwani Ukerewe yalivyomezwa ziwani

MICHEZO YANGA SC, CHIVAVIRO KIMEELEWEKA UK.24 KATUNI UK.6



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, akitoa ufafanuzi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Saturn, Rahmarullah Habib (kushoto), alipokagua ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha malori aina ya HOWO, kilichoko Kigamboni jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndugulile na Mkurugenzi Mtendaji mwenza wa kampuni hiyo, Chirag Tanna. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Samia kumsaidia Profesa Jay

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema yupo tayari kulipia gharama za upandikizaji figo kwa aliyekuwa Mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, kokote atakakotaka kwenda kupata matibabu hayo ya kibingwa.

Vilevile, Rais Samia amechangia Sh. milioni 50 kwenye Taasisi ya Profesa Jay, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada anazozifanya katika taasisi yake hiyo.

Usiku wa kuamkia jana jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alieleza hayo alipozindua Taasisi ya Profesa Jay, akisema tayari wameshapewa maagizo toka kwa Rais Samia kuhusu msanii huyo wa nyimbo za kizazi kipya aliyetamba na nyimbo mbalimbali zikiwamo 'Zali za Mentali' na 'Nikusaidiaje'.

Dk. Mollel alisema kuwa Rais Samia alihoji baada ya Profesa Jay kwenda India kwa ajili ya matibabu na kurudi Tanzania anahudumiwaje.

"Ametuelekeza kuanzia Jumanne (leo) tukutane pale Muhimbili tujadili namna nzuri ya kuhakikisha kwamba wewe (Profesa Jay) upo salama.

"Hayo ni maelekezo, Rais akishauliza Profesa Jay tulimpompeleka nje ya nchi kutibiwa, amesindikizwa na daktari, amerudi yupo hapa Tanzania.

"Hivi huduma nyingine anazoendelea, anapata matatizo, maana yake tunakutana ili tuweze kuja na mwafaka mzuri ili wewe unayeendesha hii foundation (taasisi) salama na maono yako yaweze kufikiwa kwa ajili ya watu wengine," alisema.

Naibu Waziri Mollel alisema Rais Samia amewataka kuendelea kuharakisha mchakato wa upandikizaji figo.

"Tanzania tunaweza kufanya, Mlongazila (Hospitali ya Taifa Muhimbili) wanafanya na (Hospitali ya) Benjamin Mkapa wanafanya, lakini ikitokea kuna jambo ambalo teknolojia yake haipo nchini, usiogope Profesa Jay, Rais wetu yupo pamoja na wewe, utakwenda kokote duniani kutibiwa na wewe mwenyewe unalijua hilo," aliahidi.

Dk. Mollel alisema ni vigumu kupata fedha kwa ajili ya matibabu ya maradhi hayo, akisisitiza kuwa alichokianzisha Profesa Jay kwa kuanzisha taasisi ni jambo zuri na wote wanapaswa kumpa ushirikiano.

Alisema atakuwa pamoja na Profesa Jay kwa ajili ya kutafuta fedha, wakishirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi ambaye kupitia maandiko yake, watapata mchango na kuunga mkono jambo hilo ili kuwasaidia wenye hilo tatizo.

Dk. Mollel alisema ni vizuri watu kuwa na bima ya afya, akibainisha kwa kuwa serikali inaingia gharama ya kusamehe matibabu ya wagonjwa; wastani wa Sh. bilioni 667 kwa mwaka.

"Ndio maana tunasema twende kwa Bima ya Afya Kwa Wote, tuwe tunachangiana. Kwenye eneo la figo na moyo pekee, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umetumia Sh. bilioni 789 kutibu magonjwa hayo mawili, maana yake tiba ni gharama," alifafanua.

Profesa Jay ambaye kabla ya kuibuka na wazo la kuanzisha taasisi hiyo, alilazwa siku 462 MNH, aliwashukuru Watanzania kwa kuendelea kujitoa, Rais Samia akiwa mstari wa mbele kumpigania. Aliweka wazi kuwa amepokea ujumbe kutoka kwa katibu wake kwamba atachangia Sh. milioni 50 katika taasisi yake.

"Rais Samia anaendelea kutushika mkono na inaonesha jinsi gani jambo hili ni la kitaifa na linawahusu watu wote bila kuangalia vyama, itikadi na dini.

"Ninawashukuru nyote mliojitoa bila kumsahau Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, ujumbe wake nimeupata," alisema.

Prof. Jay alisema kuwa juzi ilikuwa siku muhimu kwa uzinduzi wa taasisi hiyo kwa ajili ya kushughulika na mambo mbalimbali na walipanga waanze na maradhi ya figo kwa kuwa ni ugonjwa uliomsumbua kwa miaka miwili.

"Nimeshuhudia Watanzania wengi wakiteseka na wengi wakishindwa kumudu gharama za matibabu ya ugonjwa wa figo. Wagonjwa wengi wanarudi nyumbani wakiwa wamekata tamaa.

"Hii programu yetu mpya ya kurudisha tabasamu kwa wale waliokata tamaa, wanaoumwa na wale ambao hawana uwezo, tuwashike mkono," alisema.

Prof. Jay alisema walipanga kukusanya Sh. milioni 800 kwa kuanza na wagonjwa 50 ambao kwa wiki moja, mmoja anapatiwa matibabu mara nne ambayo kwa siku ni Sh. 300,000.

"Tunawaomba Watanzania waendelee kutushika mkono ili tuweze kuwafikia watu wengi zaidi. Mpaka sasa tuna watu 600 wanatuomba msaada, wako mikoani wanategemea Taasisi ya Profesa Jay kama mwokozi wao," alisema.

Profesa Jay aliweka angalizo kuwa kuna watu wanadhani ugonjwa wa figo unawapata watu wazima, hasa wazee, lakini ana ushuhuda wa watoto ambao wanazaliwa figo zikiwa hazifanyi kazi. Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Janabi, alisema zipo dalili 15 za ugonjwa huo na wengi wao wanazisubiri hadi wazione ndipo watambue wana tatizo la figo. Wanakuwa wameshachelewa kuanza matibabu.

"Dalili hizo ni kuchokachoka ambapo huwezi kuelezea, kulala usiku inakuwa shida, huwezi kufikiria, mwili kuwasha, miguu kuvimba unapoamka asubuhi tazama kwenye kioo unaweza kuona uso wako upo wa duara na siku zinavyokwenda unapotea," alisema.

Prof. Janabi alitaja dalili zingine ni kukosa uwezo wa kutambua ladha ya chakula, harufu ya kinywa kuwa mbaya, tumbo kuuma, kwenda haja ndogo mara kwa mara usiku na haja ndogo kuwa na povu ama rangi ya brauni.

Pia alisema kisukari ni ugonjwa unaosababishwa na ulaji mbaya wa chakula, pia husababisha ugonjwa wa figo, akihimiza kila mmoja kujitahidi kupima afya yake na kubadili mfumo wa vyakula ili kujiepusha na magonjwa.

"Watoto wadogo tunawapandikiza figo mtoto amezaliwa na kilo nne, ndugu wakija wanasema mashallah, hakuna!" alionya.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, alisema alitegemea kuona Profesa Jay anatembea, lakini alishtuka kumwona akiwa anasukumwa kwenye kiti mwendo.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema alipokuwa anamtembelea Muhimbili alikolazwa kwa muda mrefu, "aliona ukuu wa Mungu ", akisisitiza Mungu amemfanyia wema mpaka kufikia katika hali hiyo.

# Nape atangaza msako wa wazushi kifo cha Mpango

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema serikali imeanza kuwatafuta waliohusika kuzua taharuki katika mitandao ya kijamii na kutoa taarifa za uongo kumhusu Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Vilevile, Jeshi la Polisi limesema linaendelea na uchunguzi dhidi ya waliohusika kumzushia kifo kiongozi huyo, huku likionya wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii.

Kwa zaidi ya mwezi mmoja hadi juzi Makamu wa Rais alipojitokeza kanisani, kumekuwa na mjadala katika mitandao ya kijamii, wengi wakihoji kutoonekana kwa kiongozi huyo.

Akizungumza juzi baada ya kumalizika ibada ya Jumapili kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska huko Kiwanja cha Ndege mkoani Dodoma, Dk. Mpango alisema alikuwa nje ya nchi kutekeleza kazi maalum huku akionesha kukerwa na baadhi ya watu kutumia mitandao vibaya kwa kuzua taharuki, wakidai amefariki dunia.

Makamu wa Rais alisema matumizi yasiyofaa ya mitandao ya kijamii yamekuwa yanaumiza watu wengi, hivyo yampasa kila mmoja kutumia vyema mitandao hiyo na kuwa na hofu ya Mungu.

Waziri Nape katika akaunti yake ya mtandao wa kijamii wa X, alisema jana kuwa waliohusika kuzusha taarifa hizo za uongo kumhusu Makamu wa Rais, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ili kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao hiyo.

"Pole sana Mhe. Makamu wa Rais. Tumekusikia. Kwa kuwa tuna sheria zinazoelekeza mitandao itumike vizuri na kwa kuwa tuna taasisi na watu wa kusimamia sheria hizi, bila kuathiri uhuru wa mtu, tutachukua hatua kutokomeza matumizi haya mabaya ya mtandao! Naamini wote watatuelewa.

"Nimeelekeza vyombo vyote vinavyohusika, kuchukua hatua za mfano, ili tujenge jamii inayoheshimu uhuru wa kila mtu. Uhuru wowote unaoingilia uhuru wa mwingine ni uvunjaji wa sheria, hatuwezi kujenga jamii inayoona hilo ni jambo la kawaida," alisema.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa simu jana baada ya kutafutwa kujiridhisha kuhusu taarifa yake hiyo, Waziri Nape alisema matumizi salama ya mtandao ni muhimu katika kuhakikisha amani na usalama wa nchi vinakuwapo.

"Matumizi mabaya ya mtandao yanaweza kusababisha taharuki na hata kuhatarisha amani na utulivu wa nchi. Kutoa taarifa za uzushi wa kifo kwa wananchi kunaweza kuchochea hofu na wasiwasi kwa jamii," alisema.

Nape alisema kutoa taarifa na kuzusha kifo kwa mtu yeyote ni ukiukwaji wa heshima na utu wa mtu na kunaweza kuathiri maisha na kuleta mtafaruku usio na sababu.

"Matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii yanaweza kutumiwa kwa urahisi kutengeneza na kusambaza habari potofu na za uongo. Kumzushia mtu kifo ni mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumika kudanganya umma na kusababisha machafuko.

"Tunalazimika kama serikali kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wanaovunja sheria za matumizi salama ya mtandao.

"Kwa kufanya hivyo, tutajenga jamii inayoheshimu mawasiliano na inayofanya kazi kwa pamoja kwa ajili ya maendeleo na amani ya nchi," alisema.

Nape ambaye ni Mbunge wa Mtama, alisisitiza umuhimu wa kuheshimu na kulinda usalama wa viongozi na wananchi kwa kuhakikisha watumiaji mitandao ya kijamii wanaheshimu maadili, sheria na kanuni za matumizi ya mawasiliano ikiwamo mitandao hiyo ya kijamii.

"Matumizi mabaya ya mtandao yanaweza kuwa tishio kwa usalama wa wananchi. Kutoa taarifa za uongo za kifo cha mtu kunaweza kusababisha taharuki kwa familia, ndugu na jamaa zake na wananchi kwa ujumla, hivyo ni muhimu kuchukua hatua za kuzuia matendo kama haya," alisema.

Waziri huyo alisisitiza umuhimu wa serikali kuweka mazingira salama ya mawasiliano nchini ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi salama ya mtandao.

"Tunaweza kujenga mazingira salama ya mawasiliano ambayo yanawawezesha wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru bila kutumia njia za uongo na chuki kwa nia ya kudhalilisha na kuleta taharuki kwa jamii," alihitimisha mazungumzo hayo na mwandishi wa Nipashe.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), David Misime, alisema tayari jambo hilo linaendelea kufanyiwa kazi na jeshi hilo.

"Tunatoa wito kwa wale wenye nia zao ovu, waache kutumia vibaya mitandao ya kijamii kwani mkono wa sheria lazima utawafikia," alionya Kamishna Misime.

# Afariki kwa kujimwagia mafuta na kujichoma moto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MTU mmoja mkazi wa Mtaa wa Nduka, Kata ya Chamwino jijini Dodoma, Rehema Shabani (41), amefariki duniani kwa kujimwagia mafuta ya taa na kujiwasha moto akiwa amejifungia chumbani kwake.

Tukio hilo lilitokea jana majira ya saa nne asubuhi huku chanzo kikiwa bado hakijafahamika.

Akizungumza na waandishi wa habari, mama wa marehemu Suzana David, alisema jana asubuhi aliamka mapema kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya nyumbani.

Alisema mtoto wake kabla ya umauti kumfika alikuwa akiumwa kwa muda mrefu hali ambayo wakati mwingine ilikuwa ikimfanya kuchanganyikiwa.

"Alikuwa anaumwa kabla ya tukio hili hali ambayo ilikuwa inamfanya wakati mwingine kuwa kama mtu aliyechanganyikiwa na wakati mwingine kuwa sawa.

"Leo niliamka asubuhi yeye akiwa amelala, lakini badaye aliamka na kuniuliza mama unapika uji nikasema ndiyo akasema sawa akaondoka akaenda dukani baadaye akarudi baada ya kukuta duka limefungwa na kisha kurejea tena dukani," alisema.

Alisema aliporudi toka dukani aliamua kumpelekea uji chumbani kwake, lakini jambo la kushangaza alikuta mlango umefungwa.

"Baada ya kumaliza kupika uji nilimpelekea chumbani kwake lakini kufungua mlango ukawa umefungwa nikaanza kugonga mlango na kuita baadaye mpangaji wetu akatoka akasema mama mbona kuna moshi unatoka chumbani ndio kuanza kupiga makelele na kuita watu kuja kutusaidia kuvunja mlango," alisema.

Shuhuda wa tukio hilo, Issa Jafari, alisema baada ya kuvunja mlango waliingia ndani, lakini walishindwa kuona kitu kutokana na moshi mzito.

"Tuliamua kutoka nje na kupanda juu ya paa ili kung'oa bati ndipo moshi ulipopungua na kumwona Rehema akiwa ameungua moto ndani ya chumba akiwa bado hajakata roho, lakini tukaogopa kuutoa nje mwili kwa sababu polisi walikuwa hawajafika," alisema Jafari.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Nduka, Mohamed Pampai, alisema alifika eneo la tukio baada ya kupigiwa simu kuwa kuna tukio la moto katika moja ya nyumba zilizopo katika mtaa wake.

"Nilipigiwa simu hapa kuwa kuna tukio la moto limetokea, lakini nilivyofika nilikuta tayari watu wa Jeshi la Zimamoto wameshafika na nilipoingia ndani tuliukuta mwili wa marehemu ukiwa umeungua kwa moto," alisema.

Akielezea tukio hilo Ofisa Opereshoni wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma, Deogratius Inano, alisema walipata taarifa kuna nyumba inaungua na kufika kwa wakati huku wakikuta nyumba ya vyumba tisa ikiwa inaungua.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mwenzetu huyu amejichoma moto mwenyewe kutokana na ushahidi tulioukuta ndani ya chumba ikiwamo kiberiti na yeye mwili wake unanukia mafuta ya taa aliyojimwagia," alisema.

# PBPA yaokoa bilioni 425/- msongamano meli za mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umesema umeokoa zaidi ya Sh. bilioni 425 kwa kupunguza msongamano wa meli bandarini baada ya kuimarisha Mfumo wa Uingizaji Mafuta kwa Pamoja wa Mafuta nchini (BPS).

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta Pamoja (PBPA), Erasto Simon, alisema hayo jana wakati wa kikao kazi na waandishi wa habari na wahariri kilichofanyika jijini Dar es Salaam, chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuulezea umma, mafanikio na changamoto katika utelekezaji wa majukumu yao.

Alisema kila mwezi wanaokoa Sh. bilioni 4.1 kwa kudhibiti upotevu wa mafuta kwenye meli na mahala ya kuhifadhi nishati hiyo nchini.

"Mfumo huu umesaidia kupunguza msongamano wa meli bandarini katika hili wastani wa Sh. bilioni 425 huokolewa kila mwaka ikilinganishwa na gharama za zilizokuwa kabla BPS kuanza kutumika," alisema.

Kuhusu uwezo wa maghala ya kuhifadhi mafuta, alisema Tanzania ina maghala 22 yenye uwezo wa kuhifadhi mafuta yanayoingia nchini.

Alisema maghala hayo yana uwezo wa kupokea takribani lita bilioni 1.31 za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na ya taa.

Alifafanua kuwa katika Bandari ya Dar es Salaam kwa upande wa Kurasini kuna maghala 11 yenye uwezo wa kupokea takribani lita milioni 570, Kigamboni manane, lita milioni 522.

Katika Bandari ya Mtwara mawili yenye uwezo wa kupokea takribani lita milioni 35 na Bandari ya Tanga moja lenye uwezo wa kupokea takriban lita milioni 182.

Alisema serikali, inaendelea kuhamasisha wawekezaji kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta ili kuhifadhi kiwango kikubwa cha nishati hiyo nchini.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta nchini, ni lazima kuwe na hifadhi ya mafuta ya siku 15 ili inapotokea tatizo lolote nchi isiweze kupata mtikisiko.

Alisema katika mikataba ya uagizaji wa mafuta nchini, wakala hutumia tathmini ya bei ya soko inayofanywa Kampuni ya S&P Global yenye ofisini yake nchini Afrika Kusini ambayo hutumiwa na nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika kupata tathmini bei ya mafuta katika Soko la Dunia.

"Kampuni zote zinazofanya biashara ya mafuta nchini na nchi jirani hutumia tathmini ya kampuni hii katika kujua bei za mafuta kwenye Soko la Dunia," alisema na kuongeza:

"Pia kampuni mbalimbali zinazoendesha biashara au kutegemea kuwekeza katika Soko la Afrika hutumia tathmini za S&P Global kupima kiwango cha mitaji ya uwekezaji wao."

Alisema pamoja na mafanikio makubwa ya mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja, kuna changamoto kadhaa katika uendeshaji wake, ikiwamo wakati wa kipindi cha UVIKO-19, mahitaji ya mafuta yalipungua kutokana na kusimama shughuli nyingi za kiuchumi na kusababisha meli kutumika kama hifadhi za mafuta, hali ilileta uhaba wa meli za usafirishaji kuongezeka na bei ya nishati hiyo kuporomoka kwa kiwango kikubwa.

Hata hivyo, alisema wakala wake kupitia Wizara ya Nishati imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Benki Kuu Tanzania (BoT), kupunguza makali ya uhaba wa Dola za Marekani kwa kufanya baadhi ya maamuzi na na kuleta unafuu.

Maamuzi hayo ni pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kumpata mkandarasi atayeboresha miundombinu ya upokeaji mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na kutarajia kusaini mkataba mwezi huu.

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

**CAUTIONARY NOTICE TO MEMBERS**

**TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY (DSE: TCPLC)**

*(Incorporated in the United Republic of Tanzania) ("Tanga" or "the Company")*

In accordance with the rule 74(6) of the Dar es Salaam Stock Exchange Rules, companies are required to publish a cautionary notice as soon as they are satisfied that a reasonable degree of certainty exists that the financial results for the period to be reported upon next will differ by at least 25% from the financial results for the previous corresponding period.

Accordingly, shareholders are advised that Tanga Cement PLC expects that the Operating Profit before Interest and Tax for the quarter ended 30 September 2023 to be between 300% and 280% higher than that achieved in the comparative quarter ended 30 September 2022.

The contributing factors to this movement were the diligent implementation of cost-cutting strategies in maintenance and operations management, in line with the company's drive for enhanced efficiency.

The Group also expects a loss before tax for the three months ended 30 September 2023 to be between 905% and 920% higher than that achieved in the comparative quarter ended 30 September 2022. The contributing factors to this movement being higher interest expenses on term loans and foreign exchange losses, influenced by the weakening Tanzanian Shilling against the US Dollar

The company expects to publish its unaudited financial results for the quarter ended 30 September 2023 by no later than 11 December 2023.

Shareholders are accordingly advised to exercise caution when trading with the company's securities.
The financial information on which this trading statement is based has not been audited by Tanga Cement PLC's auditors.

**On behalf of the Board.**

**Hakan Gurdal**
Chairman of the Board

Jali AFYA yako
Hakiki kinywaji chako kwa kutumia App






Kwa maelezo zaidi piga simu bure
0800-780078/0800-750075
/0800-110016

# Maisha mapya ya Ukerewe makazi, mashamba yao yakimezwa na ziwa

## •Kina cha maji chaongezeka kwa mita 1.6
## •Ni rekodi ya juu zaidi tangu mwaka 1965



Mkazi Joshua Kanumba wa kijijini Selema, Ukerewe, akionesha maji ya ziwa yalivyomharibia nyumba yake. **PICHA ZOTE: SANULA ATHANAS**

**Na Sanula Athanas aliyekuwa** UKEREWE

TAZAMA maisha mapya ya wakazi wa kisiwa cha Ukerewe, mkoani Mwanza:

Mahali walipolima mahindi, mpunga, viazi na mihogo, sasa maji ya Ziwa Victoria yanakupwa na kujaa; waliokuwa wanapata milo mitatu kwa siku, sasa hawana uhakika wa kupata hata mmoja.

Miti ya machungwa na maembe iliyoiingizia halmashauri Sh. milioni 103 mwaka 2021/22 kutokana na tozo za mazao, imenyauka. Wakulima wameikata na kutengeneza kuni na mkaa. Halmashauri imelazimika kuwagawia miche mipya inayovumilia ukame.

Wilaya yao ambayo milongo mitatu iliyopita ilikuwa inalisha Jiji la Mwanza na miji ya Bunda na Musoma kwa nafaka na matunda, sasa imegeuka tegemezi; kila siku kuna wastani wa malori matatu hadi manne yanayopeleka nafaka kisiwani Ukerewe.

Makazi yaliyokuwa karibu na mwalo, sasa 'yamemezwa' na maji ya ziwa ambalo kina chake nacho kimepanda kwa mita 1.6; rekodi ya juu zaidi ya ongezeko la maji ziwani tangu mwaka 1965.

Yustina Mafuru (38), mama wa watoto wanane wanaojumuisha mabinti watatu, pia mtoto mkubwa ana miaka 17 na mdogo wao wa mwisho ana miaka mitatu, ni miongoni mwa wakazi wa Ukerewe waliopoteza mashamba.

Sababu kuu inatajwa ni kuongezeka kina cha maji ziwani. Mama huyo, mkazi wa kitongoji cha Azimio, kijijini Masonga, kata ya Kakukuru, anaifafanulia Nipashe kwa sauti ya upole na uso uliokosa tabasamu:

"Nilipoolewa mwaka 2002, nilianza kulima hapa (anaonesha kwa ishara ya mkono). Tulikuwa na shamba hapa la eka(ri) mbili na nusu. Tulikuwa tunalima mahindi, mihogo na viazi. Kwa kweli tulivuna mno, lakini mwaka juzi (2021), shamba lilimezwa na maji.

"Sasa tumeathirika sana kiuchumi, tumekosa chakula! Kama unavyoona ninatangatanga tu kupata chakula kwa ajili ya familia.

"Mume wangu ni mvuvi, hata sasa yuko ziwani na wenzake wanatafuta samaki. Akipata fedha ananipatia, ninakodi hili shamba dogo hapa (Sh. 70,000 kwa ekari), ninalima na kupata chakula kidogo kwa ajili ya wanangu.

"Kwa kifupi, maisha yetu hapa kwa sasa ni magumu mno. Wewe (mwaandishi wa Nipashe) uko karibu na serikali huko, waambie watusaidie huku. Hali ni mbaya.

"Zamani nilikuwa ninalima na kupata mazao mengi, ninauza baadhi ya mazao kupata fedha za kununulia mahitaji ya shule ya wanangu, lakini sasa sina tena cha kuuza."

Mwenyekiti wa Kijiji cha Masonga, Richard Msafiri ambaye wajihi wake kiumri ni kama Yustina, anatoa ufafanuzi kuhusu adha hiyo, akitumia mfano hai wa shamba la mkulima, Mzee Musomi Lusato, aliyestawisha migomba ekari moja kwenye mazingira ya mwaloni, lakini sasa eneo hilo halina mazao. Limegeuka sehemu ya mwalo usiokuwa na kitu.

"Baada ya mvua kubwa kunyesha mwaka 2020 na 2021, shughuli za uzalishaji shambani hazipo tena. Shamba limemezwa na maji ya ziwa.

"Kulikuwa na majirani zake wengine waliokuwa wanalima mahindi, viazi na bustani ya mboga lakini ndio hivyo tena, mashamba yamemezwa na ziwa," Msafiri anasema.



Ndio hadithi anayoendelea kusimulia ya ekari kadhaa za mpunga, mahindi na viazi, hali kadhalika mgahawa na miundombinu ya wavuvi waliyoitumia kukutana na kupumzika, vyote vimetoweka kwa nguvu ya maji.

"Hapa (akionesha kwa mkono) palikuwa na kambi za wavuvi, walijenga vibanda vyao vya muda. Pia palikuwa na mgahawa pale, wavuvi walipata huduma katika mgahawa huo, lakini sasa huwezi kuamini kwamba pale palikuwa na mgahawa.

"Kuna mti huu wa kihistoria, ulipandwa miaka ya 1980 na Mzee Joshua Kabuche (marehemu). Ulikuwa mbali mno na ziwa, lakini mwaka juzi (2021), maji yaliufikia, ukaanguka," anasimulia.

Mwenyekiti Msafiri anaeleza hatua za kujihami kwa maisha yajayo, wametoa hadhari wakazi wa kijiji hicho chenye vitongoji vitano vya Azimio, Bugando, Kirumba, Maendeleo na Butiama, wasiendeshe tena kilimo kwenye eneo hilo la karibu na mwalo kwa maana kuna ishara ya hasara zijazo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kakukuru, Obadia Maega, anaeleza jitihada za ofisi yao kiserikali ni tahadhari ya kutojenga kwenye maeneo ya karibu na mwalo, wakiwa na ushuhuda wa yaliyojiri.

Joshua Kayumba (53) ni mvuvi aliyefikwa na mkasa wa makazi kumezwa na ziwa katika kijiji cha Selema, kata ya Bwiro. Yu mwandamizi wa shughuli za ziwani. Hata makazi yake amekuwa akipunga upepo wa ziwani, hatua kadhaa toka barazani.

Leo analalama makazi yao ya ufukweni yamebaki hadithi. Nyumba moja imetolewa na kishindo hicho cha mwaka 2021, nyingine aliyoijenga kwa Sh. milioni 22, hata inamtoa machozi, imebakia nusu na kwa hatari iliyopo, amekwishahama mahali hapo.

Akigeuka nyuma, ana familia. Ni baba wa watoto 23. Kati yao, 15 anaishi nao alikopanga hivi sasa katika makazi salama na wake zake wawili kijijini Selema.

Kwa hadhi yake ya baba wa familia, anapaswa kuwawezesha wote dhidi ya magumu yote ya kimaisha anayotamka ni mizani nzito inayotitirisha machozi yake.

Nini kilitokea? Bila kutaja siku wala tarehe, Kayumba anakumbuka ilikuwa majira ya jioni, alisikia kitu mithili ya dhoruba ziwani, upepo unavuma na dalili zote za hali ya hewa kutokwenda sawa, kigezo kikuu ni uzoefu wake ziwani.

Hatua ya kwanza ya 'zimamoto' ilikuwa kuhamisha wanafamilia waliokuwamo katika nyumba zote mbili, wakatafuta mahali pengine pa kujisitiri. Na kadri muda ulivyosonga, maji ya ziwa yalizidi kusogelea nyumba zake, ambazo awali zilikuwa umbali wa mita 70 toka mwaloni.

Kayumba anasema hali ya dhoruba ilizidi kusonga nyumbani kwake, mwisho wa hadithi makazi na vifaa vya uvuvi alivyoviacha ndani ya nyumba vikasambaratishwa.

Anasema hata ahueni ilipopatikana, akarejea mahali hapo kutoka 'uhamishoni' kukagua kilichojiri mwaloni, akakumbana na jibu la uhalisia kuharibika kwa nyumba zake na vifaa vyake vya uvuvi, mtaji unaompa maisha ya kila siku.

Anaisimulia Nipashe, hata kilimo cha magimbi na matikiti wastani wa ekari moja na nusu karibu na makazi yake, ambacho mapato yake yalikuwa si haba kwa familia, nacho kikafika mwisho. Wamehamia rasmi kwenye maisha magumu.

"Kwa ujumla, hali imebadilika. Utafutaji umekuwa mgumu kwenye maji. Maisha yetu yanazidi kuwa magumu. Maji nayo yameingia ndani ya nyumba na kuondoka na kila kitu," analalama Kanumba.

Adha hiyo haiko kata ya Bwiro pekee. Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Muritilima, kata ya Kakukuru, Fabian Mtaki anasema kijiji chake chenye vitongoji saba, nacho kimekumbwa na adha hiyo. Vyote viko karibu na ziwa.

Mtaki anasema kitongoji cha Makutano kimeathiriwa zaidi. Nyumba nne zimeanguka pamoja na vibanda vya wafanyabiashara. Soko la Samaki la

**Inaendelea uk. 10**



Mkazi wa Kijiji cha Masonga, Ukerewe, Yustina Mafuru, akionesha lililokuwa shamba lake, baada ya kuharibiwa na maji ya ziwa.

# Makamu wa Rais Z'bar apigia chapuo Kiswahili kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema diplomasia ni mlango mkubwa na muhimu katika kuendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili kimataifa.

Othman aliyemwakilisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi, aliyasema hayo alipokuwa akifunga kongamano la saba la kimataifa la lugha ya Kiswahili.

Alizitaka taasisi zanazosimamia lugha ya Kiswahili Tanzania Bara na Zanzibar kutumia vyema diplomasia ili isaidie kuimarisha lugha hiyo.

Pia aliyataka mabaraza hayo kutumia mbinu nzuri ya kusambaza Kiswahili kwa kuandaa na kuchapisha vitabu vya lugha hiyo na kuifundisha kwa weledi pamoja na kujenga uhusiano na ushirikiano wa kukuza lugha hiyo katika mataifa mbalimbali duniani.

Aidha, alisema Kaulimbiu 'Kiswahili ni Zaidi ya Lugha tukitumie kuimarisha demokrasia," hakuna budi kutumika kuimarisha diplomasia inasisitiza haja kwa jamii ya watumiaji wa lugha hiyo duniani kuungana na mabaraza ya Kiswahili Tanzania ili kuendeleza, kukuza na kuisambaza zaidi lugha hiyo.

Aliyataka Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), kuendelee kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa wageni ndani na nje ya nchi kwa kuwa hatua hiyo itasaidia kupata walimu wenye uzoefu na utaalamu utakaorahisisha lugha hiyo kufundishwa kwa umahiri ziadi.

Aidha, alisema umefika wakati kwa Balozi za Tanzania zilizopo nje kuhamasisha usomeshaji wa lugha ya Kiswahili katika mataifa wanayowakilisha nchi hatua ikayosaidia waliopatiwa mafunzo kuzitumia fursa za kusomesha Kiswahili ndani ya nchi hizo.

Alisema ni wajibu wa serikali kujitahidi kuunga mkono juhudi za kuendelezwa lugha ya Kiswahili zinazofanywa za usomeshwaji ndani na nje ya nchi ambazo kuna wazungumzaji zaidi ya milioni 200 duniani na kwamba lazima diplomasia itumike katika kukiimarisha.

Alitoa wito kwa vyombo mbalimbali kuhakikisha vinakitumia Kiswahili katika uasili wake pamoja la kuienzi lugha hiyo ambayo ni jukwaa na ukumbi wa pekee wa hadhara ya Waafrika wote ili kuendelea kuutunza na kuuhifadhi utamaduni wa Waswahili na Waafrika kwa jumla.

Aidha, aliwataka wasomi na wabobezi na wataalamu wa lugha ya Kiswahili nchini kuweka mkazo kwa kufanya utafiti ili pamoja na mambo mengine kubaini iwapo kuna tishio, mkwamo na changamoto zozote dhidi ya Kiswahili pamoja na kufikiria suluhisho au njia bora za kuendeleza lugha hiyo.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema kuna haja ya kuzifanyia kazi changamano za misamiati ya Kiswahili zinazojitokeza kwa watumiaji mbalimbali wa lugha hiyo ili iweze kutumika kwa ufasaha.

Alitaka kuendelezwa vijana wanaojifunza ushairi ili kuwa wenye ujuzi na utaalamu zaidi kuitumia vyema lugha hiyo kwa mazingira tofauti.

Katibu Mtendaji wa BAKIZA, Dk. Mwanahija Ali Juma, alisema kongamano hilo lililowashirikisha wahadhiri wa vyuo vikuu, wanadiplomasia kutoka ndani na nje ya Tanzania pamoja na wanafunzi wa vyuo limeazimia kutumia Kiswahili katika maandishi mbalimbali na kutafsiri kazi za lugha nyingine kusaidia ajira na wasiojua Kiingereza wapate kupitia tafsiri pamoja na kuajiri walimu wa Kiswahili kuwapeleka nje wafundishe lugha hiyo.

## NEMC yaonya wanaoishi pembeni mwa fukwe, mito

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wananchi kuepuka maeneo ya fukwe za bahari, mito na maziwa ili kuepuka madhara ya mvua.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa baraza hilo, Menan Jangu, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mvua inayoendelea kunyesha.

Alisema wananchi wanaoishi kando ya milima wanapaswa kuchukua tahadhari kubwa kwa kuwa kuna uwezekano wa kutokea maporomoko ya udongo na kusababisha athari kwa maisha ya watu.

Aliwataka madereva wa vyombo vya moto kuchukua tahadhari wakati wa safari kwa kuzingatia kuwa maeneo ya barabara yanaweza yakawa siyo salama.

Pia, wamiliki wa maeneo ya uchimbaji na uchenjuaji wa madini kwenye mabwawa ya majitaka yenye tope sumu na maeneo ya kutunzia miamba ya sumu kuhakikisha maeneo hayo hayaleti madhara kwa jamii na vyanzo vya habari.

Kwa kipindi cha miezi miwili maeneo mbalimbali yamekumbwa na mvua ambazo zimeleta athari kubwa ikiwa ni pamoja na maafa yaliyojitokeza katika maeneo ya Katesh, wilayani Hanang katika Mkoa wa Manyara.

Aidha, alisema taarifa kutoka katika Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) zinaonesha kuwa mvua ya viwango tofauti itaendelea katika maeneo mbalimbali nchini na imekuwa kubwa na kuendelea kusababisha madhara.

Alisema mvua hiyo imesababisha mafuriko kwenye maeneo mbalimbali hali iliyosababisha madhara kama vile makazi kuharibiwa na wananchi kukosa maeneo ya kujisitiri na wananchi kupoteza maisha na wengine kuumia baada ya kuchukuliwa na mafuriko.

"Miundombinu ya maji na barabara kwenye baadhi ya maeneo imeathirika na kupelekea huduma za usafiri kukwama, usalama wa maji kuathiriwa kutokana na mwingiliano wa maji yasiyo salama yanayotokana na mafuriko na maji ya matumizi ya nyumbani hivyo kusababisha magonjwa ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na magonjwa ya mlipuko," alisema .

Alisema eneo lingine la kuzingatiwa ni miundombinu ya kuhifadhi majitaka na topesumu kwenye migodi na kwamba mvua inayoendelea kusababisha miundombinu husika kujaa na mingine kuvujisha maji yenye sumu na kuathiri mazingira na hata mifugo kupoteza maisha kwa baadhi ya maeneo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi wa kujengea nyumba waathirika ni wa kupongezwa

**WAATHIRIKA** wa maafa ya maporomoko ya tope yaliyosababishwa na mvua wilayani Hanang', mkoani Manyara, sasa watajengewa nyumba ili warejee katika maisha yao ya awali.

Uamuzi huo wa serikali umetokana na michango inayoendelea kukusanywa kutoka kwa mashirika ya umma na wadau mbalimbali waliojitokeza kutoa misaada ya hali na mali kuwasaidia wananchi hao waliopata madhara.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotangazwa, jumla ya kaya 107 zilizokuwa na wakazi 322 zimepoteza makazi katika mji wa Katesh, vijiji vya Jorodom, Ganama, Katesh, Dumbeta, Gendabi, Sarijanda, Arukushay na Sebasi baada ya maporomoko ya mawe, magogo na matope yaliyosababishwa na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia Desemba 3, mwaka huu.

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan, alikabidhiwa hundi ya Shilingi bilioni mbili kutoka kwa Msajili wa Hazina, Nehemia Mchechu, kwa ajili ya msaada kwa waathirika hao.

Moyo wa Watanzania kusaidia wenzao waliokumbwa na mafuriko hayo, unawapa imani na matumaini ya kuendelea na maisha baada ya baadhi ya waathirika hao kupoteza kila kitu na kuachwa wakiwa hawana mahapa pa kuishi.

Utaratibu wa kuwajengea nyumba utawapa faraja kubwa kutokana na maafa waliyoyapata kuanza kujenga makazi mapya yangewachukua muda mrefu na wengine wasingeweza kumudu.

Hata hivyo, angalizo katika kuwafariji waathirika hao, kusiwe na upendeleo kwasababu hakuna aliyetarajia kuwa angepatwa na maafa hayo.

Wakati akipokea msaada wa hundi hiyo, Rais Samia alisema ujenzi wa nyumba na misaada mingine inayotolewa ikiwamo vifaa vya ndani, vyakula na huduma za afya ni faraja kubwa kwa wananchi hao wanaopitia kipindi kigumu cha kupoteza ndugu na mali zao.

Rais Samia amesema kwa michango hiyo hakuna kitakachozuia kwenda kujenga nyumba kwa operesheni za haraka nyumba za Shilingi milioni 25 au milioni 30 ili waathirika hao warudishwe katika maeneo yao.

Majanga yanatokana na mazingira hayawezi kuzuilika na hakuna mtu anayeweza kumlaumu mwingine cha msingi ni kuishi kwa tahadhari huku wananchi wakipewa elimu ya kuepuka kuishi karibu na maeneo yanayoonekana kuwa hatarishi kwao.

Vilevile, ni muhimu kwa wananchi kujifunza kutunza mazingira badala ya kuyaharibu ili kuepuka majanga ambayo yanaweza kuzuilika.

Pale inapotolewa elimu kuwa sehemu ambazo hazitakiwi wananchi kujenga basi isichukuliwe kuwa wananyanyaswa hiyo ni kwa faida yao ili kuepuka na majanga yanayoweza kudhibitiwa.


Kuna maeneo ambayo yalikuwa njia ya kupita maji, lakini wananchi wameyavamia kwa kujenga nyumba jambo ambalo ni hatari kwasababu kwa mvua hii inayoendelea kunyesha ambayo tangu mwezi wa nane, Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) ilitoa tahadhari, yanaweza kuamua kupitia kwenye ushoroba wake na kusababisha majanga makubwa.

Tumeshuhudia maeneo kadhaa nchini yakiathirika kutokana na wananchi kuamua kuvamia na kujenga makazi ya kudumu. Jambo hili ni hatari kwasababu maji yana nguvu kubwa na yanatisha.

Wananchi pia ni lazima wawe makini wanapokatazwa wasipite eneo fulani kwa tahadhari ya maisha yao wasikilize badala ya kulazimisha na matokeo yake ni kusababisha vifo.

Ni matumaini yetu kuwa faraja hii ya kujengewa nyumba wananchi waliopoteza makazi yao itawarudishia matumaini ya kuendelea na maisha kama kawaida.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hii imulikwe kukomesha mimba kwa wanafunzi

**MIKOA** ya Songwe, Ruvuma, Katavu, Mara na Rukwa, inatajwa kuwa na viwango vikubwa vya mimba za utotoni, hatua hiyo inaweza kuwa ni tishio kwa maendeleo ya elimu kwa wanafunzi wa kike iwapo jitihada zaidi za kukabiliana na mimba hizo hazitachukuliwa.

Kwa mfano, wakati akizindua Ripoti ya Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania ya mwaka 2022 hivi karibuni, Rais Samia Suluhu Hassan, anaweka wazi kila kitu.

Anasema, pamoja na Tanzania kupunguza viwango vya mimba za utotoni, kutoka asilimia 27 mwaka 2015/16 hadi asilimia 22 mwaka 2022, bado kuna haja ya kuongeza jitihada za kupunguza viwango hivyo, ili kuwalinda watoto wa kike.

Rais Samia anasema, Mkoa wa Songwe una asilimia 45 ya kiwango cha mimba za utotoni, ukifuatiwa na Ruvuma kwa asilimia 37, Katavi asilimia 34, Mara asilimia 31 na Rukwa asilimia 30.

Wakati mikoa hiyo ikiwa na kiwango hicho, Rais anasema mkoa wa Dar es Salaam mimba zimeongezeka kutoka asilimia 11.9 hadi asilimia 18.1, huku mkoa Njombe nao ukitajwa kuwa na kasi ya mimba hizo kutoka asilimia 19.7 za awali hadi kufikia 25.5.

Ninadhani kwa takwimu hizo, kuna haja mikoa hiyo kumulikwa zaidi kwa kuchukua hatua mbalimbali zitakazosaidia kukomesha mimba kwa wanafunzi, ili waweza kutimiza ndoto zao katika elimu.

**Ninadhani kwa takwimu hizo, kuna haja mikoa hiyo kumulikwa zaidi kwa kuchukua hatua mbalimbali zitakazosaidia kukomesha mimba kwa wanafunzi, ili waweza kutimiza ndoto zao katika elimu.**

Kwa ujumla ni kwamba, mimba shuleni limekuwa ni tatizo sugu, wanafunzi wamekuwa wakirubuniwa na vijana wa mtaani, wazee na hata walimu wao na kusababisha wakatishe ndoto zao katika somo.

Tatizo hilo linatajwa kuchangia zaidi na mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii kuanzia ngazi ya familia, kutokana na baadhi ya wazazi na walezi kushindwa kuwapa malezi bora watoto wao tangu hatua ya awali hivyo kukosa msingi bora wa maadili.

Lakini wanafunzi wa kike nao wanatajwa kusumbuliwa na tamaa ya kutaka kumiliki vitu vizuri na kujikuta wakijiingiza katika mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo na watu mbalimbali ili kutimiza haja zao.

Vilevile jamii inayowazunguka, nayo imekuwa ikitamani kutembea na watoto wa shule ikiamini wao ndio wako salama na hawana maambukizi ya magonjwa ya zinaa ukiwamo UKIMWI.

Aidha, tamaa ya walimu kwa wanafunzi au wanafunzi kwa walimu pia. Ninadhani njia mojawapo ya kudhibiti hayo yote, ni wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia kuendelea kushirikiana na serikali katika vita hiyo.

Wakati mwingine kumekuwapo taarifa za walimu kuoa wanafunzi wao mara tu baada ya kuhitimu elimu ya msingi au sekondari. Kitendo ambacho ni mwendelezo wa mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii.

Hivyo mikoa yenye kiwango kikubwa cha mimba kwa wanafunzi na mazingira yote hatari kwa wanafunzi au watoto wa kike yangemulikwa zaidi kwa kuwekewa mikakati ya kudhibiti ukatili huo wa kijinsia.

Njia mojawapo zinazoweza kutumika, ni serikali kutoa adhabu kali wale wanaobainika kuwapa ujauzito wanafunzi, lakini pia ni vyema wanafunzi wakapewa elimu ya jinsia na mahusiano shuleni.

Hatua hiyo inaweza kusaidia walimu kuwa na ujasiri wa kutoa elimu hiyo, kwani baadhi yao husita wakihofia jamii kuipokea vizuri kutokana na imani kwamba kuwafundisha elimu hiyo ni kuwachochea kuingia masuala ya mahusiano ya kimapenzi.

Kuendelea kuwapo kwa mimba za utotoni au kwa wanafunzi, ni sawa na kuendeleza ukatili wa kijinsia ambao umetengewa siku 16 kila mwaka kwa ajili ya kupambana nao lakini bado hauishi.

# Serikali kusikiliza malalamiko ya kodi

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imewaita wadau mbalimbali wakiwamo wafanyabiashara na Watanzania wenye matatizo ya kikodi kuyapeleka kwenye Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (TOST) ili wapatiwe suluhu.

Taasisi hiyo mpya ilianzishwa 2019 kwa marekebisho yaliyofanywa katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2015, ambayo ujenzi wa mifumo yake ulianza Februari, mwaka huu. Sasa ni chombo huru kilichoundwa chini ya Wizara ya Fedha.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati wa utambulisho rasmi wa TOST, Mkuu wa taasisi hiyo, Robert Manyama, alibainisha kuwa sababu ya kuanzishwa chombo hicho ni kutoa jukwaa huru lenye usawa wa kutatua malalamiko dhidi ya usimamizi wa sheria za kodi kwa njia ya majadiliano na upatanishi.

"Kuharakisha utatuzi wa malalamiko kwa kutumia taratibu zisizo na gharama kubwa au kuhitaji utumiaji wa wanasheria. Na kujenga imani ya walipakodi kwa mfumo wa usimamizi na ukuusanyaji wa kodi nchini ili kuchochea utii wa hiyari wa sheria na taratibu za kodi," alisema Manyama.

Kadhalika, sababu nyingine ni kuhakikisha kwamba ukiukwaji wa taratibu za usimamizi wa sheria za kodi unaodaiwa kufanywa na mamlaka za kodi unaangaliwa na taasisi huru kwa nia ya kumshauri Waziri wa Fedha hatua za kurekebisha. Nyingine ni kutumia mbinu za upatanishi katika kutatua changamoto za malalamiko ya kodi ambazo huimarisha uhusiano baina ya walipa kodi na watoza kodi, na kuhakikisha uwazi, na urahisi katika kushughulikia malalamiko ya kodi, hivyo kutoa mazingira rafiki kwa ajili ya kutatua malalamiko ya kikodi.

Aidha, ushirikishaji wa pande zote zenye mgogoro kwa kiwango cha juu zaidi cha kuheshimiana na kuaminiana kwa nia ya kufikia muafaka kwa malalamiko ya kodi.

Alisema sababu nyingine ni kushirikisha mamlaka katika jitihada za kuzuia kwa kupitia ukiukwaji wa taratibu za kodi na malalamiko ya kodi yaliyotolewa taarifa kwa nia ya kuwa makini na kuwezesha usimamizi thabiti wa sheria za kodi.

Aidha, alibainisha kuwa vigezo vya kuwasilisha malalamiko TOST, ni pamoja na mlalamikaji awe hakupokea majibu yoyote ndani ya siku 30 kutoka kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tangu kuwasilisha malalamiko lake, na endapo mlalamikaji hakuridhishwa na majibu ya TRA.

"Lalamiko lazima liwe limetokea ndani ya siku 90 na endapo ni zaidi ya muda huo mlalamikaji anatakiwa kutoa sababu zitakazomridhisha msuluhishi kabla ya kupokelewa," alisema Manyama.

Hata hivyo, alisema shauri linalolalamikiwa halihusiani na lililowahi kusuluhishwa na ofisi ya usuluhishi isipokuwa kama kuna ushahidi au taarifa mpya zinazoweza kuathiri uamuzi wa awali.

Vile vile, alibainisha kuwa malalamiko ya kodi yanayoshughulikiwa na TOST ni yanayohusu taratibu, huduma na masuala ya kiutawala ambayo yalikuwa yanadaiwa kinyume na utaratibu katika usimamizi wa sheria za kodi.

Alisema kingine ni mamlaka kukiuka wajibu wake katika mkataba wa huduma kwa mlipa kodi wakati wa kutoa huduma.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa TOST, Edwini Iwato, alisema taasisi hiyo pia ina jukumu la kuzingatia usawa na haki kwa wote. Pamoja na kudumisha usiri, kuhusiana na kila malalamiko yaliyopokelewa, isipokuwa inapohitajika na sheria.

# Balozi Ufaransa asifu mradi kuwabaini wenye saratani

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, amesema kuanzishwa mradi wa Tanzania Comprehensive Cancer Care (TCCP) kumesaidia kwa kiasi kikubwa kuwabaini wenye ugonjwa wa saratani na kuanza matibabu kwa wakati.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam alipokutana wadau wa huduma ya afya Aga Khan Tanzania (AKHS-T) na Taasisi ya Curie ya Ufaransa, wakiadhimisha miaka minne ya ushirikiano katika mradi wa TCCP.

Alisema watu 700,000 wamepimwa ili kugundua kama wana saratani katika hatua za awali ambapo asilimia 28 ya wagonjwa wamegundulika mapema na kupatiwa matibabu kwa wakati."Kuanzishwa kwa huu mradi, watumishi wa afya 330 wamepatiwa mafunzo ya huduma ya saratani, na wananchi milioni 4.5 wamepatiwa elimu ili kuongeza uelewa kuhusiana na ugonjwa wa saratani," alibainisha.

Balozi huyo alisema kuwa tangu kuanzishwa mradi huo unaolenga kukabili changamoto inayoongezeka ya magonjwa yasiyoambukiza nchini, ifikapo mwakani kituo kipya cha matibabu ya saratani kitazinduliwa jijini Dar es Salaam ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Maendeleo ya Ufaransa (AFD) C'eline Robert, alisema wamekuwa wanafanya kazi bega kwa bega kuwajengea uwezo wadau wote hasa kwenye ugonjwa wa saratani kwenye tiba ya mionzi, mipango ya uchunguzi na kuziwezesha hospitali za umma na binafsi za saratani nchini.

Mkurugenzi wa Tiba katika Hospitali ya Agakhan, Dk. Harrison Chuwa, alisema mradi huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuwaibua wenye saratani na kuwapatia matibabu.

"Mradi huu umenipa fursa ya kuwaibua wagonjwa wenye saratani. Changamoto iliyopo ni uelewa. Baadhi yao wanadhani wamerogwa na kujikuta wakiendelea kupata madhara zaidi," alisema.

Dk. Chuwa alisema mradi huo ulipoanza mwaka 2020, asilimia 85 ya wagonjwa walikuwa kwenye hatua ya tatu na ya nne. Walichelewa kuanza matibabu.

Alisema takwimu za hadi Oktoba 30, mwaka huu, zinaonesha asilimia 31 ya wagonjwa wa saratani wanafika hospitali wakiwa kwenye hatua ya kwanza na ya pili na kuanzishiwa tiba, hivyo ni muhimu wananchi kupima afya zao na kuanza matibabu kwa wakati badala ya kuchelewa kuanza tiba.


# TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD; TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED** na **MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD,** kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku Kumi na nne (14) na Siku Saba (7) kama rudio la tangazo kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SALUM OMARI AMIRI | SALUM OMARI AMIRI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MWANDEGE, VIKINDU KATA YA MKURANGA | 21/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD |
| 2 | NOBLE REAL ESTATE | YUSUPH MWINULA GEORGE | C.T NO. DSMT 1027706 PLOT NO P31713 | GOBA AREA, KINONDONI | 06/01/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| | | YUSUPH MWINULA GEORGE | C.T NO. DSMT 1005641 P5401 | NYAKASANGWE KINONDONI | 06/01/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | |
| 3 | PATRICIA ANURUPHUS MPANJU | ANURUPHUS MPANJU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MADALE, WAZO MANISPAA YA KINONDONI | 19/12/2023, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | | |
|---|---|---|
| **LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD P.O.Box 68172**<br>**Dar es Salaam, Tanzania**<br>**Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559**<br>**Email: lehalelglc@gmail.com** | **TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**<br>**P.O.BOX 1305**<br>**Songea, Ruvuma**<br>**Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298 / 0784 718 734**<br>**Email: twinscoltd5@gmail.com** | **MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD**<br>**P.O.Box 12943**<br>**Arusha, Tanzania**<br>**Tel: 0752 632 033/ 0628512033**<br>**Email: mangwembe@gmail.com** |

177535

# Samaki wapandikizwa katika bwawa la mgodi lililobomoka

Na Marco Maduhu, KISHAPU

BWAWA jipya la Mwang'olo lililojengwa na mgodi wa madini ya almasi (WDL) wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga limepandikizwa vifaranga 5,000 vya samaki aina ya sato ikiwa ni sehemu ya kurejesha hali ya awali ya bwawa lililobomoka kingo zake mwishoni mwa mwaka jana.

Awali bwawa lililobomoka lilikuwa na mazalia ya samaki, waliowasaidia wakazi wa maeneo hayo kujishughulisha na uvuvi. Mgodi huo umeamua kupandikiza samaki wengine ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali la kurudisha bwawa hilo katika hali yake ya awali.

Meneja Uhusiano mgodi huo, Bernard Mihayo, akizungumza wakati wa upandikizaji huo, alisema agizo la serikali ni kurudisha kila kitu ambacho kiliharibika baada ya kupasuka kwa bwawa la majitope la mgodi wao Novemba mwaka jana na kuleta madhara kwa wananchi.

"Tayari tumekamilisha ulipaji fidia kwa waathirika. Tunachokifanya sasa ni kuhakikisha tunarudisha hali ya mazingira kama ilivyokuwa awali ikiwa ni pamoja na kupanda miti.

"Vilevile, tunapandikiza vifaranga hawa ili wananchi waendelee na shughuli zao kama kawaida ikiwamo uvuvi wa samaki na kuinuka kiuchumi na kupata kitoweo kama ilivyokuwa awali," alisema Mihayo.

Alitaja vifaranga 5,000 vimepandikizwa. Katika kuhifadhi mazingira ya eneo hilo, tayari wamepanda miti 10,000 na upandaji miti utakuwa endelevu kuhakikisha eneo hilo linarejea katika asili yake.

Ofisa Uvuvi Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Moses Ng'winza, aliwataka wakazi wa eneo hilo kusubiri hadi miezi sita ipite ndipo samaki hao wawe tayari kwa shughuli za uvuvi. Serikali itatoa elimu na maelekezo kuhusu uvuvi katika eneo hilo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Fatma Mohamed, aliwataka wananchi kuendelea kulitunza bwawa hilo na kila mmoja awe mlinzi wa mwezake, pia akikemea kilimo karibu na bwawa hilo.




Ofisa Uendeshaji Mkuu Benki ya CRDB, Bruce Mwile, akipokea Cheti cha Ubora cha Usimamizi wa Huduma za TEHAMA cha ISO 20000-1:2018 kutoka kwa Mkurugenzi Mkaazi na Mkuu wa Sera za Biashara na Uwekezaji, British High Commission, Anna-Maria Mbwette, ambaye amekabidhi kwa niaba ya Shirika la Viwango la Uingereza (BSI) katika hafla fupi iliyofanyika jana, Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB yapata cheti cha ISO usimamizi huduma TEHAMA

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya ya CRDB imekabidhiwa cheti cha viwango vya Usimamizi wa Huduma za TEHAMA cha ISO 20000-1:2018 kilichotolewa na Shirika la Viwango la Uingereza (BSI).

Cheti hicho kilikabidhiwa jana katika hafla fupi iliyofanyika makao makuu ya benki yaliyoko barabara ya Ali Hassan Mwinyi jijini Dar es Salaam.

Akipokea cheti hicho kutoka kwa Mkurugenzi Mkaazi ambaye ni Mkuu wa Sera za Biashara na Uwekezaji Ubalozi wa Uingereza, Ofisa Uendeshaji Mkuu wa Benki ya CRDB alisema cheti hicho ni ishara ya dhamira ya dhati ya benki yao katika kuhakikisha mifumo, taratibu na huduma za TEHAMA za benki zinakidhi ubora wa kimataifa.

Mwile alisema benki ya CRDB imekuwa inawekeza katika mifumo ya kisasa na hivyo kupelekea mabadiliko makubwa katika huduma zake za TEHAMA kufikia viwango vya kimataifa.

Alisema mazingira ya biashara yamekuwa yanabadilika kwa kasi kutokana na ukuaji wa teknolojia, jambo ambalo limepelekea benki hiyo kufanya mchakato wa kuboresha viwango vyake.

"Tukitambua umuhimu wa kuwa na mifumo ya utoaji huduma iliyo na viwango bora, benki ilifanya mchakato wa kupata cheti cha ubora wa ISO 20000 cha usimamizi wa huduma. Tulipitia mchakato mrefu uliohusisha uboreshaji michakato yetu ya usimamizi wa huduma za TEHAMA," alisema.

Mwile aliongeza kuwa benki hiyo pia iliwekeza mipango ya kina ya mafunzo na uhamasishaji ili kuhakikisha wafanyakazi wanaelewa mahitaji ya viwango vya ISO 20000 na kutambua majukumu yao muhimu katika michakato ya usimamizi wa huduma za TEHAMA. Ilikwenda sambamba na kuanzishwa utamaduni wa kuboreha mifumo ya TEHAMA mara kwa mara.

Akielezea faida za kupata uthibitisho wa kiwango hicho cha kimataifa cha ISO, Mwile alisema kunasaidia kuchochea michakato na taratibu zinazohakikisha huduma za TEHAMA zinatolewa kwa ufanisi na kukidhi viwango vya kimataifa, hivyo kutoa uzoefu ulio bora kwa wateja.

"ISO 20000 pia inakuza utamaduni wa kuboresha mara kwa mara. Cheti hiki kinatuhimiza kutathmini na kurekebisha mara kwa mara michakato yetu ya usimamizi wa huduma za TEHAMA, kuhakikisha tunaendana na mabadiliko ya mahitaji ya wateja na maendeleo ya teknolojia," alisema.

Akikabidhi cheti hicho, Mkurugenzi Mkaazi na Mkuu wa Sera za Biashara na Uwekezaji Ubalozi wa Uingereza, Anna-Maria Mbwette, aliipongeza Benki ya CRDB kwa cheti hicho cha ubora wa kimataifa na kusema kunaonesha dhamira yake katika ubora, usalama na usimamizi madhubuti.

Anna-Maria alisema kupata ISO 20000 katika huduma za TEHAMA kutasaidia benki hiyo kujenga imani si tu kwa wateja wake, bali pia wawekezaji na washirika wa kimataifa kwa kuwa viwango hivyo vinatambulika na kutumika kote duniani.

Kiwango cha ubora wa ISO 20000 katika usimamizi wa huduma za TEHAMA ni mwendelezo wa jitihada za benki ya CRDB katika kufikia viwango vya kimataifa kwa kuwa benki hiyo tayari imepata vyeti vya ubora vya ISO/IEC 27001:2013 cha usimamizi wa usalama wa taarifa na ISO 22301:2019 cha mipango, mifumo na michakato ya uendeshaji biashara yenye ufanisi.

# Bilioni 6/- zakarabati miundombinu ya elimu

Na Halima Ikunji, URAMBO

WILAYA ya Urambo, mkoani Tabora imepokea Sh. bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu ya awali, msingi na sekondari.

Fungu hilo limetolewa na serikali kwa lengo la kukabili uhaba unaotishia ustawi wa elimu wilayani humu.

Mkuu wa Wilaya ya Urambo, Elibariki Bajuta, ofisini kwake juzi alimwambia mwandishi wa habari hizi kuwa fedha hizo zilipokewa kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema fedha hizo zimetumika katika ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wasichana, nyumba za walimu na Shule mpya Msingi Samia, inayoanzia elimu ya awali.

"Mabweni manne yamejengwa katika Shule ya Sekondari Urambo na nyumba nne za walimu katika Shule ya Sekondari Kasisi.

"Ni uamuzi ambao umeendelea kuboresha elimu ya msingi na sekondari wilayani hapa huku kazi ikibaki kwetu kama jamii kuitunza miundombinu hii," alisema Bajuta.

Kuhusu sekta ya afya, Mkuu wa Wilaya alisema huduma zimeboreshwa kwa serikali kutoa zaidi ya Sh. bilioni 2.5 kusogeza huduma za afya karibu na wananchi na kudhibiti vifo vya mama na mtoto.

Alisema kwa sasa vituo vya afya vitatu viko katika hatua tofauti ambavyo ni Kituo cha Afya Vumilia, Songambele na Ukondamoyo ambayo vinatarajiwa kuanza kutoa huduma mwakani.

Alibainisha kuwa wilaya ina zahanati 18 zinazofanya kazi, sita zingine ziko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji ujenzi wake na tayari fedha zimetolewa na serikali kuhakikisha zinakamilika na kuanza kutoa huduma.

Vilevile, alisema kuwa katika Hospitali ya Wilaya walipokea Sh. milioni 900 kwa ajili ya kuboresha miundombinu yake ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo ya huduma za dharura, mionzi, mama, baba na mtoto, na jengo la upasuaji.

## Mkemia Mkuu ahadharisha wadau uhifadhi wa kemikali

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, ameagiza wadau wote wanaojishughulisha na kemikali, kuhakikisha wanatimiza wajibu wa kulinda afya za binadamu na mazingira.

Alitoa maagizo hayo jana jijini Arusha alipofunga mafunzo ya siku tatu yaliyoshirikisha viongozi wa sekta binafsi na taasisi za serikali 148 wanaojishughulisha na kemikali.

Dk. Mafuniko alisema mafunzo hayo yametolewa na ofisi yake kwa lengo la kujenga ufahamu kuhusu Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inavyoendesha shughuli za usimamizi na udhibiti wa kemikali.

"Tunachosisitiza kwao hasa kwa hawa viongozi tunaowapatia mafunzo haya, wafahamu vizuri Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali pamoja na kanuni zake za mwaka 2020, ili watimize wajibu wao bila kuleta madhara kwa afya za binadamu na mazingira, sababu watakuwa wanafahamu sheria inataka nini," alisema.

Aliongeza kuwa endapo kila mdau atafuata na kuzingatia vizuri sheria hiyo, itawasaidia kuchochea biashara zao kufanyika kwa ufasaha na kwa kulinda afya za binadamu na mazingira.

"Hapa tuna maana hata wale wanaosafirisha kemikali kutoka nje ya nchi na wasambazaji wote lazima wawe na kibali, ili wafanye shughuli za kemikali bila kuleta athari na hili ndilo lengo letu sisi katika ofisi yangu," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Ofisi ya Mkemi Mkuu wa Serikali, Magdalena Mtenga, alisema mafunzo hayo yanashirikisha washiriki 148 kutoka sekta binafsi na taasisi za serikali, wakiwamo wadau kutoka nchi jirani ya Kenya na Uganda.

Alisema kuwa mbali na kuwaelimisha kuhusu sheria ya kemikali na kanuni zake, pia wamezungumzia masuala mbalimbali ya mikataba ya kimataifa na kuhimiza umuhimu wa kufanya biashara hiyo kwa kufuata sheria na kanuni zake, ili kuepuka athari kwa afya ya binadamu na mazingira.

"Pia tumewakumbusha umuhimu wa kusimamia utekelezaji salama wa makasha ya kuhifadhi kemikali pale kemikali zinapoisha kutumika na kuhakikisha hayatumiki kwa kuweka bidhaa zingine ili kulinda afya za binadamu," alisema.

**"Tunachosisitiza kwao hasa kwa hawa viongozi tunaowapatia mafunzo haya, wafahamu vizuri Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali**

# Wachimbaji wazipa msaada familia zilizokumbwa na mafuriko Mirerani

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WACHIMBAJI wakubwa wa madini ya Tanzanite wametoa misaada kwa waathirika wa mafuriko ya mvua za El-Nino katika kata za Msitu wa Tembo na Shambarai zilizoko mji mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Misaada hiyo ya kibinadamu ikiwamo vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni 31, imetolewa na Kampuni ya Franone Mining LTD inayomiliki kitalu C katika machimbo ya Tanzanite, Mirerani.

Jana, Mkurugenzi wa Kampuni ya Franone Mining LTD, Onesmo Mbise, kabla ya kukabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alisema wametoa msaada huo baada ya kusikia waathirika hao wanahitaji msaada. Mbise alivitaja vyakula walivyotoa ni magunia 200 ya mahindi, katoni 40 za mafuta ya kupikia, magunia 40 ya maharage na mifuko 20 ya sukari.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), sisi kama Kampuni ya Franone, tunashirikiana na jamii inayotuzunguka, ndio sababu tuliposikia watu wa Msitu wa Tembo na Shambarai wamekumbana na adha hii ya mafuriko, tukaona tusaidie vyakula hivi," alisema Mbise.

Baada ya makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya, Dk. Suleiman Serera, aliishukuru kampuni hiyo kwa kutoa msaada huo kwa waathirika wa mafuriko yaliyotokea eneo hilo.

Alisema baadhi ya waathirika nyumba zao zimebomoka kutokana na mafuriko hayo na wengine vyakula vyao vimeharibika. Msaada huo ni faraja kwao.

"Maeneo yalioathirika sana kwenye wilaya yetu ni vijiji vitatu vya Shambarai, Orbili na Kilombero katika kata ya Shambarai na Kijiji cha Londoto kilichoko Kata ya Msitu wa Tembo," alisema Dk. Serera.

Akitoa shukrani kwa niaba ya wananchi wake, Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alipongeza kampuni hiyo kwa kuwachangia waathirika wa mafuriko hayo.

Ole Sendeka alisema Franone Mining LTD imekuwa msaada mkubwa kwa jamii kwa kuwa hivi karibuni wakati wa ukame ilisaidia chakula kwa shule mbili za kata ya Naisinyai.

"Franone Mining LTD tunawashukuru kwa mengi, pia mlisaidia kutoa Sh. milioni 60 kwa kata za Endiamtu na Naisinyai na mmetumia Sh. milioni 140 kwa jamii, hongereni kwa moyo wenu wa kujitolea," alipongeza Ole Sendeka.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Asia Ngaliwason, waliokumbwa na mafuriko hayo ni watu 126 kutoka kaya 49.




Baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Azania wakiwa kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Tanzania Desemba 9. Lengo ni kufikisha huduma za Azania kwenye kilele cha mlima huo na kuleta chachu katika sekta ya utalii nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tarehe kuanza sera mpya ya elimu, mafunzo yatangazwa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imetangaza rasmi kuwa kuanzia Januari 8 mwaka ujao, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023 iliyofanyiwa mabadiliko na kuridhiwa na Rais Samia Suluhu Hassan, itaanza kutumika.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. James Mdoe, alisema elimu ya lazima ya miaka 10, itaanza kuhesabika kuanzia Januari mwaka 2024 kwa ngazi ya darasa la awali (chekechea), darasa la tatu na kidato cha kwanza ambacho kitakuwa na mikondo miwili ya amali (ufundi) na mkondo wa kawaida wa jumla.

Prof. Mdoe alikuwa anazungumza na wanazuoni na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) wakati wa hafla ya kukabidhi tuzo kwa waliofanya vizuri zaidi kwenye masomo, uongozi na michezo.

Akifafanua zaidi kuhusu elimu ya lazima ya miaka 10, Naibu Waziri huyo alisema: "Sasa hivi tuna sera mpya inayoitwa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la Mwaka 2023. Kuidhinishwa kwa sera hii, maana yake tunakuja na mabadiliko ya mitaala, ambayo tulikuwa tunaiandaa kwa ajili ya kuanzia elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari ya chini, elimu ya sekondari ya juu na vyuo vya ualimu.

"Elimu ya lazima ya miaka 10, maana yake ni kwamba, ni miaka sita ya elimu ya msingi, na miaka minne ya elimu ya sekondari ya chini. Januari 2024, chekechea wataanza na mtaala mpya, darasa la tatu wataanza na mtaala mpya, kidato cha kwanza itakuwa na mikondo miwili ya mkondo wa amali (ufundi) na mkondo wa kawaida wa jumla.

"Mwaka 2024, hatutaanza na mkondo wa jumla, kwa kidato cha kwanza ila tutaanza na amali kwa shule chache, na nyingine ni zile ambazo sasa hivi zinafanya mafunzo haya yanayoendana na amali, kwa mfano Tanga Technical School, Moshi Technical School, Ifunda Technical Shool na Mbeya Technical School.

"Lakini, ikifika 2025, tutaongeza tena shule nyingine na kadhalika. Na ikifika 2025, tutaanza sasa hata mtaala mpya kwa kidato cha kwanza."

Kuhusu tuzo hizo, Prof. Mdoe alisisitiza kwa menejimenti ya MoCU kuweka malengo na kuyasimamia vizuri.

Pia alishauri wanafunzi kutambua kwamba wao ni watu wa kuigwa na wenzao walioko madarasa ya nyuma, hivyo wayaishi mafanikio waliyoyafikia.

Makamu Mkuu wa MoCU, Prof. Alfred Sife, alisema katika tuzo hizo, mwanafunzi bora aliyefanya vizuri katika masomo ya Shahada ya Udaktari wa Falsafa (Phd), Dk. Petro Nzowa, amepewa zawadi ya Sh. 700,000.



RIPOTI MAALUM

# Maisha mapya ya Ukerewe makazi, mashamba yao yakimezwa na ziwa

**Inatoka uk. 4**



Mwenyekiti wa Kijiji cha Masonga, Ukerewe, Richard Msafiri, akieleza jambo kuhusu madhara ya kutanuka maji ya ziwani Victoria.

Kata ya Kakukuru nalo limepomolewa upande na maji ya ziwa yaliyolifikia. Wanakijiji wameshauriwa wahame kwenye maeneo hayo.

"Tumewashauri wakajenge kwenye maeneo ambayo hayawezi kuathiriwa kiurahisi. Lile eneo (kitongoji cha Makutano) lina ardhi oevu, linatuamisha maji. Wengi wameanza kuhama kuelekea ardhi ya juu.

**WATAALAMU SERIKALINI**

Akianza na ushuhuda, mwandishi alipotua kisiwani Ukerewe tarehe 7 ya mwezi uliopita, alikutana na tukio lililotikisa kisiwani; mkazi mwanamke kufariki dunia Novemba 4, mwaka huu kutokana na kupigwa radi katika Kijiji cha Kameya, kilichoko kata ya Nduruma.

Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Elias Maziku, anatoa tafsiri pana ya mazingira kisiwani humo, akisema mvua kubwa isiyoendana na kalenda inayojulikana, ikimbatana na radi na upepo mkali, imekuwa na athari ya moja kwa moja kwao.

Anasema hali hiyo imedhuru uchumi wa wakazi, ikiwamo kusababisha mafuriko yanayobomoa nyumba na mazalia ya samaki ziwani, ilhali uvuvi ndio mwajiri mkuu wa wakazi.

Pia anafafanua kuwa baada ya mvua kubwa kunyesha katika kalenda isiyotarajiwa, kumekuwa kukitokea ukame unaoathiri shughuli za kilimo ambacho ni mwajiri namba mbili na mlishaji mkuu wa wakazi, akiyataja maeneo ya Gana, Maliasili, Monarch, Bwiro, Masonga, Kamasi na Muritilima kuathiriwa zaidi na mafuriko ya mwaka 2021.

Maziku anasema imefikia hatua Ukerewe sasa ndio inayolishwa badala ya sifa yake ya awali kulisha Jiji la Mwanza kwa nafaka na matunda, hata miji jirani ya Bunda na Musoma.

Anatumia mfano wa kielelezo kidogo namna utajiri wa kuzalisha nafaka Ukerewe kulisha majirani, sasa yenyewe inalishwa kwa wastani wa malori matatu hadi manne yanayogonga hodi kisiwani kila siku yakibeba nafaka kwa ajili ya wenyeji.

Ofisa Mazingira huyo anathibitisha kile anacholalamika mvuvi Kayumba kwamba wakazi wengi sasa hawana uhakika wa lishe, pia sifa ya milo mitatu kwa binadamu kwa siku, wasifu huo unahama rasmi Ukerewe.

Maziku anasema hayo ni matokeo ya athari za mabadiliko ya tabianchi, waathirika wakuu wakiwa ni wanawake na watoto.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Hermina Minja, katika hilo analalamika kuwapo upungufu wa chakula kama vile mahindi, mihogo, mpunga na viazi vitamu ambavyo awali vilizalishwa kwa wingi.

Kukabiliana na tatizo lililojitokeza mwaka jana la wakazi kukata miti ya maembe na machungwa iliyoyauka kutokana na ukame, Hermina anasema halmashauri imegawa kwa wananchi miche mipya inayovumilia ukame huku yenyewe ikianzisha shamba lake, ikipanda miche 10,000. Uwekezaji huo umegharimu Sh. milioni 30.

**MZIZI WA TATIZO**

Mtaalamu Mbobezi wa Jiolojia, Dk. Peter Kafumu, anaanza kwa kutambulisha silaha ya kwanza kukabili matatizo kama hayo ya Ukerewe, ni kuzingatia hatua zote za tahadhari zinazowasilishwa na mamlaka husika kitaifa na kimataifa.



Anafafanua kwamba kinachojiri Ukerewe na kwingineko Afrika Mashariki, ni matokeo ya ongezeko la joto juu ya wastani katika eneo la kati la Bahari ya Pasifiki.

Kijiografia bahari hiyo iko kati ya Amerika upande wa mashariki na Bara la Asia/ Australia upande wa magharibi. Ina ukubwa wa kilometa za mraba milioni 179.7 ambazo si tu ni bahari kubwa, bali pia ni eneo kubwa kuliko nchi kavu yote duniani; ni karibu nusu ya uso wa dunia.

Katika ufafanuzi wake, Dk. Kafumu anasema panapokuwapo ongezeko la joto kwenye bahari hiyo, athari zake kijiolojia huangukia zaidi Ukanda wa Afrika Mashariki na kwingineko jirani. Ni sehemu ya sababu zinazozua balaa sasa Ukerewe na kwingineko.

Mwandishi anafika jijini Mwanza mezani kwa Jamson Edwin (pichani) Mhaidrolojia katika Kitengo cha Usimamizi wa Rasilimali Maji cha Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Viktoria (LVBWB), anayetoa ufafanuzi wa kinachoendelea Ukerewe, akitaja chanzo kikuu ni mvua kubwa iliyonyesha mwaka 2021 na kufurika mito inayoingiza maji ziwani ambayo ni pamoja na: Kagera, Mara, Mbarageti, Simiyu, Gurumeti, Nzoia na Katonga.

Athari yake, Edwin anaitaja ni kuongezeka maji ziwani; kimo kikipanda kwa mita 1.6, kikivunja rekodi zote zilizokuwapo za ongezeko la kina tangu mwaka 1965, yaani miaka 58 iliyopita.

"Kwa Ziwa Victoria tuna vituo vinne vya ufuatiliaji. Tuna kituo katika bandari za Bukoba, Mwanza, Nansio na Musoma. Katika kituo cha Bandari ya Mwanza, tuna takwimu za kuanzia mwaka 1965 mpaka sasa ambazo zinatusaidia kuratibu hali ya kina katika ziwa.

"Kina kikubwa zaidi kuwahi kutokea ni mwaka 2021 mwezi Mei, inaonesha kilifikia mita 1,134.84 kutoka usawa wa bahari ambacho kilikuwa ni sawa na ongezeko la mita 1.6 kutoka wastani wa muda mrefu uliorekodiwa mwaka 1965.

"Kutokana na ongezeko hilo lililotokea mwaka 2021, kulikuwa na madhara mbalimbali yaliyojitokeza kuzunguka Ziwa Victoria.

"Inaonekana watu wengi walijisahau, wakasogea karibu na chanzo hiki cha maji na kufanya shughuli zao ikiwamo kujenga nyumba, hoteli na kuanzisha mashamba ya kilimo.

"Kina kilipoongezeka mwaka 2021 kilisababisha maeneo yao mengi kumezwa na maji na hivyo kupata hasara kubwa. Sababu kubwa kulingana na rekodi zetu inaonekana mvua iliongezeka," anafafanua.

Mtaalamu Edwin, akiwa na mifano hiyo ya kilichotokea mwaloni; hoteli, nyumba na mashamba kumezwa na maji, anatoa ushauri kwamba wote wanaotaka kuwekeza miundombinu, iwe ya huduma, makazi au biashara, ni vyema wakaonana na wataalamu wa bodi hiyo kwanza kabla ya kuendelea na hatua zaidi.

**WASIMAMIZI MAENDELEO**

Ofisa Mapato wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Longino Ondole, anaeleza mabadiliko hayo ya tabianchi yaliwapatia makadirio tata katika makusanyo yao.

Anasema mazao ya matunda kama maembe na machungwa 'yalifurahia' ongezeko la mvua, hata mapato yake yakapanda. Mathalani mwaka wa fedha 2021/22, makadirio yalikuwa Sh. milioni 32, lakini yakawa Sh. milioni 103.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Wanchoke Chinchibera, anaungana na mtangulizi wake mwanamazingira Maziku, pia Ofisa Kilimo Hermina, kwamba kuna ugumu wa maisha, hata hesabu ya kupitisha siku kwa mwana Ukerewe sasa imekuwa ngumu.

Chinchibera anaeleza kwamba ofisi yake imekuwa inapata kesi nyingi za wazazi wa kiume na kinamama vijana waliotelekeza watoto wao, hata baadhi yao kupelekwa katika kambi maalum za kulea watoto.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Ukerewe, Mkuu wa Wilaya Hassan Bomboko, anasema hakuna fidia kwa waathirika, lakini anaorodhesha mikakati kukabili athari:

Mosi, wakazi wanapewa elimu upya kuhusu shughuli za ujenzi ufukweni, umbali usiopungua mita 60 toka majini.

Pili, utunzaji mazingira kwa kupanda miti, huku wilaya ikibuni mradi wa kupanda miti milioni mbili kufikia mwaka 2025. Hadi sasa miti 900,000 imeshaoteshwa.

Bomboko anataja hatua zingine kwamba kati ya visiwa 38 vya Ukerewe, 15 vyenye makazi ya watu vimeshaoteshewa miti ya michikichi kwa ajili ya uzalishaji mafuta.

Vilevile, Bomboko anasema wilaya yake imeanzisha mradi wa biashara ya kuvuna hewa ukaa kwa kuwa na shamba lake la miti.

Kiuchumi, Mkuu wa Wilaya Bomboko anasema kuwa baada ya kubaini wananchi wameiharibu miti yao ya matunda iliyokumbwa na ukame mwaka jana, hususan maembe na machungwa, uongozi wa wilaya umewapatia mbegu himilivu zitakazokuwa na manufaa kwao na wilaya kwa ujumla. Ni mbegu zilizozalishwa na wataalamu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

**RIPOTI LHRC**

Kile kinachojiri hivi sasa Ukerewe, kimo katika tafsiri pana ya Mkataba wa Paris 2015 ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa (UN), ambao mkono wa utekelezaji wake ndio mikutano ya kimataifa ya mabadiliko ya tabianchi inayofanyika kila mwaka.

Ndiyo mwongozo mkuu duniani hivi sasa. Namna ya utekelezaji wake inachukua sura tofauti kulingana na mazingira na wakati.

Katika hilo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kina angalizo lake kupitia Ripoti ya Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye Haki za Kijamii, Uchumi na Mazingira Tanzania kiliyoitoa Machi mwaka huu.

Kimsingi, ripoti hiyo inabainisha kuwa afya, chakula, elimu, maji safi na salama, mazingira, faragha na familia, ni haki zinazoathiriwa zaidi na mabadiliko hayo; wanaoumia zaidi ni wanawake na watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, anataja utafiti uliozaa ripoti hiyo, ulifanywa katika wilaya 10 za Tanzania Bara, ikiwamo Ukerewe, kati ya Julai na Novemba 2022.

Ripoti hiyo inataja mabadiliko hasi yako zaidi kwenye sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi, yakisababisha upatikanaji hafifu wa chakula na maji safi na salama, pia mahitaji ya shule kwa watoto.

Kuhusu nini kifanyike, Dk. Anna anashauri: "LHRC inatoa rai kwa serikali, taasisi na jamii ya Watanzania kwa umoja wetu tuchukue hatua itakayotuwezesha kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi."

Utafiti huo ulifanywa na LHRC kwenye vijiji 20 katika wilaya 10 za mikoa sita: Mwanza, Kagera, Manyara, Dodoma, Mbeya na Pwani.



Ukurasa 12

Kilio cha mwanamke mgumba, akiomba huruma na msaada



Nipashe

# TESA

Jumanne Desemba 12, 2023

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

Bwawa lililofunikwa Mwadui lilivyogeuka kisima cha fursa

ELIMU

NA SABATO KASIKA

KUHITIMISHA SIKU 16 VS UKATILI

# Wenye ulemavu pia huhitaji vyoo maalum shuleni

UNAPOMWONA mwanafunzi mwenye ulemavu wa miguu anayetembea kwa mikono, unaona huruma na kuwaza usumbufu anaoupata vyooni, kwenye usafiri na njia zenye matope.

Umeona, lakini hujachukua hatua una nafasi bado kwa sababu katika maeneo mengi hasa shule hakuna vyoo rafiki kwa wenye mahitaji.

Hawana namna hutumia huduma ya choo kwa kuchangamana na wengine wenye viungo kamili na kwenye mazingira yasiyo rafiki.

Wenye ulemavu katika Sekondari ya Jangwani, Dar es Salaam, waliokuwa katika changamoto hiyo, na sasa mambo yamebadilika.

Ni baada ya kujengewa vyoo rafiki, kazi inayofanywa na Taasisi ya Maisha ya Amani kwa Watu Wenye Ulemavu.

Shirika hilo linakabidhi vyoo rafiki vinne vilivyojengwa kwa gharama ya Shilingi milioni 20.

Mkuu wa shule hiyo, Bhoke Nyaiburi anasema ujenzi wa vyoo hivyo ni hatua nzuri ya kuwakomboa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambao awali walikuwa wakichangamana na wengine wasio na changamoto za kimaumbile kwenye huduma ya choo.

Mwalimu Bhoke anasema shule hiyo ina wanafunzi wenye ulemavu zaidi ya 100 na kwamba wana vyoo vinne vinavyoendana na hali yao.

"Vimejengwa kulingana na hali zao, wanaweza kuvitumia kirahisi bila kutishia usalama wala afya zao."

Awali walikuwa wakichangamana na wenzao wenye viungo kamili jambo ambalo halikuwa rafiki kwa wakati wote, anaongeza.

Anafurahia kuwa ni msaada unaoondoa changamoto kwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo ambao walikuwa wanapata kero zilizowasababishia karaha za kimwili na kiafya.

"Taasisi iliangalia zaidi sehemu zenye uhitaji maalum, kama kuna wanafunzi wenye ulemavu wa viungo, hivyo ujenzi wa vyoo hivi ni huduma stahiki kulingana na maumbile yao," anasema.

Anaiambia Nipashe wakati wa kukabidhiwa huduma hiyo kuwa uwapo wa vyoo hivyo unawaongezea utulivu na kujiamini, wanafunzi wenye ulemavu kwa kuachana na fikra na hisia za mazingira yasiyowapendeza na hata kuwanyong'onyeza wanapofikiria suala la kwenda maliwatoni.



Katibu Mkuu, Abeida Rashid Abdallah akiwa na wanafunzi wenye ulemavu wa Shule ya Sekondari Jangwani baada ya hafla ya kukabidhi vyoo vya wenye ulemavu. **PICHA: SABATO KASIKA**

### HAMASA KWAO

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Abeida Rashid Abdallah ambaye anaishi na ulemavu, anawataka wanafunzi wa kike wenye ulemavu wasiuchukulie kuwa ni kikwazo.

Abeida mgeni rasmi katika makabidhiano hayo, anawakumbusha wasiione hali hiyo kama kikwazo cha kutosoma na kukatisha ndoto zao za maisha, badala yake wafanye bidii zaidi wasijinyanyapae.

Anasema serikali za Muungano ya Mapinduzi Zanzibar zinafuatilia na kuweka mazingira bora ya wenye ulemavu kwenye vyombo vya uamuzi, na kwamba wenye mahitaji maalumu wasikate tamaa, kwa kuwa hawajaachwa nyuma.

"Tanzania ni nchi inayotekeleza miongozo mbalimbali inazungumzia masuala ya watu wenye ulemavu ikiwamo UN Covection on the right of People with disabilities," anasema Abeida.

Anafafanua kuwa kuna sheria ya Tanzania Bara ya mwaka 2010 wakati Zanzibar kuna sheria namba 9 ya mwaka 2006, iliyofanyiwa marekebisho mwaka jana.

Anawaambia kuwa zote zinazungumzia wajibu wa utambuzi wa haki kwa watu wenye ulemavu, usawa na kutokubaguliwa na kukuza uelewa.

Aidha, anatoa wito kwa walimu katika shule mbalimbali kuweka vyoo rafiki kwa wanafunzi wenye ulemavu, na sio vyoo tu, bali pia mazingira yawe bora kwa kundi hilo.

Kadhalika Mkurugenzi wa Taasisi ya Maisha ya Amani kwa Wenye Ulemavu, Sofia Mbeyela, anasema ujenzi wa mradi wa vyoo rafiki kwa wanafunzi wa kike wenye ulemavu ulianza Julai mwaka jana na umegharimu Shilingi milioni 20.

Sofia anasema mbali na vyoo hivyo vinne, kuna chumba kwa ajili ya wenye ulemavu kujisitiri wakati wa hedhi bila usumbufu wa kuchangamana na wengine.

"Tunawashukuru wadau waliojitolea kwa hali na mali kuchangia ujenzi huu, kwani awali shule hii ilikuwa na vyoo rafiki vitatu huku wanafunzi wakiwa 110, hali ambayo ilileta matatizo kwao, " anasema Sophia.

Anaongeza kuwa mradi huo wa ujenzi wa vyoo rafiki kwa wanafunzi walemavu utaendelea katika shule zote za sekondari za Dar es Salaam, huku akiomba wananchi, viongozi, mashirika na taasisi za umma na serikali kuendelea kuchangia.

Kuchangia ni muhimu ili kuwaondolea wanafunzi wenye ulemavu changamoto inayotokana na ukosefu wa huduma ya vyoo rafiki, anasisitiza.

Mkurugezi huyo ambaye pia ni mwenye ulemavu, anasema anaelewa changamoto zinazowakabili wanafunzi wenye ulemavu na kwamba ataendelea kupambana ili kundi hilo lisiachwe nyuma kwenye huduma muhimu.

Mmoja wa wanafunzi walemavu wa shule hiyo, Zulfa Swaleh, anayesoma kidato cha kwanza, anasema amefarijika na ujenzi wa vyoo hivyo, lakini pia anaomba wananchi kujitokeza kuwasaidia.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kilio cha mwanamke mgumba, akiomba huruma na msaada

• Wagumba huuliwa, kuporwa mali, wapo gerezani kisa kuiba watoto

MWAKA 1973 katika Kijiji cha Mtimbila, Wilaya ya Malinyi, Mkoa wa Morogoro, anazaliwa Shamira Mwakwenjula (50).

Kama ilivyo ada kupata mwenza na kufunga ndoa ni jambo la kijamii na ilipofika 1997 Shamira anaolewa, akiwa na mumewe wanatarajia kuwa na familia, japo haikuwezekana.

Baada ya miaka 11, ilipofika 2006, mumewe anamweka pembeni, akidai ameshindwa kumzalia watoto na kujenga familia, kwa vile ni mgumba.

Ripoti ya Shirika la Afya Duniani ya Aprili mwaka huu, inasema idadi kubwa ya watu duniani wameathiriwa na ugumba, takriban asilimia 17.5 ya watu wazima ambao ni sawa na mtu mmoja kati ya sita duniani hawawezi kuzaa.

WHO inasisitiza upatikanaji wa huduma za upandikizaji kwa gharama nafuu lakini za hali ya juu kwa ajili ya kuwasaidia wanaohitaji watoto ambao hawashiki mimba wala hawawezi kumpa mwanamke ujauzito.

Shamira anajua tatizo hilo ni kubwa, hayuko peke yake, hivyo anavunja ukimya na akisema mgumba si mnyonge ana haki na zaidi imetokea ni lazima aangalie mbele na kuishi maisha yake.

Anaamini kuwa katiba inasema wote ni sawa na wana haki zote kuanzia kuishi, elimu na kushiriki siasa.

"Niliposema niingie kwenye siasa nitetea haki za wasio na watoto bila kujali wanawake au wanaume, ndipo nilipofahamu kuwa mgumba hakubaliki. Niliamini wote tuna fursa sawa, lakini kumbe wapo wengine wasiotakiwa," Shamira anasema.

Anaeleza kuwa hatasahau alipokutana nacho alipoomba uenyekiti wa Kijiji cha Mtimbila na baadaye udiwani wa kata hiyo.

"Niliomba uenyekiti mwaka 2018 na ilipofika 2010 niliomba kuchaguliwa diwani wa kata ya Mtimbila, nilichokutana nacho ni kejeli, kudharauliwa na kebehi nyingi," anasema.

Mfano, anaulizwa: "Unagombea udiwani, mtoto huna, una uchungu gani na sisi hata utake kutuongoza? Huzai huna mume wala mtoto utatueleza nini mgumba wewe?"

"Tuambie utazungumziaje watoto au matatizo ya uzazi wakati hujazaa?" Ni baadhi ya 'zawadi' anazokutana nazo anapoomba uongozi wa kijiji ambao anasema aliwekwa pembeni.

Hakukata tamaa, anaingia kwenye mchuano wa udiwani wakati wa uchaguzi mkuu wa 2010, jina lake linapotoka kwenye mchujo wa wagombea anashika nafasi ya tano, hata hivyo hakuna aliyempa kura.

Anapozungumza na Nipashe wakati wa Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia na miaka 36 ya TAMWA, anasema kukosa mtoto kumemletea unyanyapaa na kudharauliwa.

"Wanaume wananifuata kila mahali kunikebehi kuanzia majukwaani hadi nyumbani naulizwa unagombea nini, hivi hujijui? Huna familia wala hadhi."

Anasema yote hayo yalimletea 'presha' shinikizo la damu, kuanguka jukwaani wakati akijieleza ili kuomba kura, lakini nyumbani alidondoka kwenye kiti na kuanguka kutokana na shinikizo hilo kumbana, akifikiria anavyodharauliwa.

Anapoulizwa iwapo aliripoti manyanyaso hayo kwenye uongozi wa chama au watetezi wa haki za binadamu, jibu ni hakujisumbua.


Shamira akizungumzia haki za wagumba na tasa. **PICHA: MWANDISHI WETU**

> Huyu ameshindwa kumpa heshima mumewe, siku hizi anaitwa baba fulani. Zamani akiwa na wewe alibakia na jina la ujana.

Anasema kwa miaka mingi ameishi na donda moyoni na sasa amefunguka, akiunda Chama cha Wagumba na Tasa Tanzania (CCWT), ambacho kina wanachama 459 kutoka mikoa mbalimbali, pia wapo wanaume 39 japo wengi hawajitokezi, wanaficha siri.

Anasema amenyanyaswa kwenye majukwaa ya kisiasa lakini kuna ukatili mwingi dhidi ya wagumba, akisema kwenye familia wakwe, waume pia wake wenza na jamii nzima, ikiwachukulia kama wasiostahili.

"Ukiwa sokoni, njiani na popote ndani ya jamii unaonekana kama hujatimia. Mfano nyumbani, mume akikufukuza akaoa, mke mwenzako atakusimanga mbele za watu, akisema.

"Huyu ameshindwa kumpa heshima mumewe, siku hizi anaitwa baba fulani. Zamani akiwa na wewe alibakia na jina la ujana."

"Tumepoteza heshima kwenye jamii na mali nyingi, kwani hata kama umechuma utajiri na mumeo ukikosa mtoto anakufukuza na kubakia na kila kitu, akiwa na pesa au ujanja ukienda mahakamani unashindwa pia."

Wagumba wanazidi kuwa maskini na hata ukiumwa unakosa msaada, wanatuhumiwa uchawi kuroga familia za waume zao, wake na watoto wao, anasema.

"Iwapo wataumwa au kufariki lawama wanaelekezewa wagumba hata kama umeachwa," kwa mujibu wa Shamira unyanyasaji huo huwalazimisha kuhama kijiji, mji au mkoa kulinda maisha huku wakipoteza mali zao.

Chama cha Wagumba na Tasa Tanzania kinajitanua sehemu mbalimbali akisema kina matawi Morogoro, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

## ANACHOTAMANI

Shamira anatamani watambulike rasmi na kutajwa kwenye wizara, halmashauri na hata katiba. Mfano, Kuna Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Katika makundi hayo kama walivyo wazee, wagane, wajane pengine watu wanaoishi na VVU na UKIMWI na wagumba watajwe kisheria kuwa ni sehemu ya 'makundi maalumu.'

"Tunatamani pia katiba mpya ianishe kuwa Tanzania kuna makundi maalumu wakiwamo wagumba ili nasi tuheshimike na kupata huduma."

Anazungumzia fedha za 4:4:2 ambazo ni asilimia nne ya wanawake, vijana na asilimia mbili kwa wenye ulemavu, akisema mgumba anaishi na upungufu kimaumbile ndiyo maana hawana watoto, lakini unapokwenda kuomba fedha hizo hapati kwa kigezo hicho hapati.

"Kama tungetambuliwa kuwa nasi ni sehemu ya makundi maalumu tungesaidiwa." Anasema.

Anahofia wagumba wananyanyapaliwa sehemu za kazi inawezekana wakaachwa kupewa baadhi ya majukumu kwa imani kuwa kwa sababu hawana watoto wanaweza kuharibu mambo.

Inawezekana hospitalini mkunga mgumba asikubalike kwa imani kuwa anaweza kufanya 'mabaya' wodi za wazazi kwasababu hana mwana.



## SHERIA YA NDOA

Sakina Isalwa ni mwanaharakati kutoka kituo cha Sauti ya Umma Mbagala jijini Dar es Salaam, kinachofanyakazi na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP)anayeeleza kuwa huenda wagumba wengi wameuawa ili kuwapora mali.

Japo, haijathibitika kiutafiti, anasema unyanyapaa kwenye jamii ni mwingi na wakati mwingine huishi peke yao na baadhi ya ndugu huwafanyia visa hata kuwamaliza ili kuchukua mali zao.

Wapo waliouwa na waume zao, wanafamilia kama ma shemeji, lakini kuna baadhi wanajiua kwa kuchoshwa na unyanyapaa na wengine kupata sonona na kurukwa na akili.

"Wanaharakati walishinda kesi waliyotaka sheria ya ndoa itambue kuwa mwenye miaka 14 ni mtoto hivyo hastahili kuoa wala kuolewa na sasa tunasubiri marekebisho. Kadhalika sheria hiyo tunatamani izungumze kitu kuhusu wagumba."

Sakina anasema sheria hiyo inatakiwa kuwazungumzia na kuziainisha haki za wanandoa wagumba kwa kuwa wananyanyaswa kijinsia, kiuchumi na kihisia.

## WIZI WA WATOTO

Mwanaharakati Sakina anasema magerezani kuna wagumba wanaotumikia adhabu kutokana na wizi wa watoto yote hayo yamewavurugia maisha yao.

"Wanaiba watoto ili kutaka kuwa na heshima kwenye jamii. Jamii inaamini kuzaa mtoto ndiyo heshima ya mwanamke. Kuitwa mama fulani ndicho wanachotaka kwani ndivyo jamii inavyoamini," anasema Sakina.

Anaungwa mkono na Latifa Somji mwanachama wa chama cha wagumba, anayesema serikali imeyatazama makundi mbalimbali ni vyema pia iwaainishe wagumba na stahili zao.

Aidha, masuala ya uchaguzi yakiainisha kuwa wagombea kama wanaoishi na ulemavu, wanawake, vijana na wagumba wajitokeze na haki zipatikane ili kuibua changamoto zao kwenye vyombo vya uamuzi.

Latifa anaamini wanawake wengi wagumba wanapitia matatizo mengi yakiwamo kupoteza maisha, kuporwa mali, kusingiziwa uchawi na sasa ni wakati wa kuwazungumzia.

## KOSA LA NANI?

Licha ya wanaume kuwalaumu wanawake kwa ugumba, wataalamu wanaeleza kuwa zaidi ya asilimia 50 ya matatizo ya kukosa watoto yanatokana na wanaume.

Wanaume ndiyo wahusika wakuu wa kufanikisha kupatikana ujauzito, anasema Mkuu wa Kitengo cha Uzazi Saidizi na upandikizaji katika Hospitali ya KCMC Dk. Tom Kikumbi.

Kikumbi mbobezi wa magonjwa ya kinamama na upandikizaji mimba, anasema licha ya ugumba kuwa tatizo kubwa nchini, kwasababu haliui (kusababishi kifo), watu hawalijali.

Anaeleza kuwa takwimu za WHO zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 50 ya matatizo ya kukosa watoto kwenye ndoa au watu wenye uhusiano kwa muda mrefu linawahusu wanaume na si wanawake kama jamii inavyoamini.

Anasema ni kweli ugumba kwa wanawake umechukuliwa kama fimbo ya kuwanyanyasa kijinsia, kiuchumi, kifursa na hata wengine hujiua lakini hakuna sababu ya kuishi kwa mazoea na kuwataka wanaume na wenzao wafike hospitalini kuchunguzwa.

## CHANZO UGUMBA

Bingwa wa tiba ya magonjwa ya kinamama na uzazi saidizi pamoja na upandikizaji, anasema kwa wanawake tatizo ni magonjwa yanayoathiri viungo vya vya uzazi.

Matatizo yanayoweza kuleta ugumba ni maradhi ya ngono kama kaswende na kisonono, lakini kukosekana uwiano wa vichocheo mwilini (hormonal imbalances), kuwa na vivimbe kwenye kizazi na mirija (fibroids).

> Wanaume wanakuwa wagumu kutafuta matibabu mfano utasikia nina UTI sugu, inawezekana ni maambukizo ya magonjwa ya zinaa. Lakini hayatibiwi yanafichwa.

Dk. Tom anazungumzia matatizo ya kuzaliwa nayo mfano kizazi kidogo, wengine wana vizazi viwili, kutoa mayai yasiyopevuka wala yasiyo na ukubwa uliokamilika ili kurutubishwa na kupata mimba.

"Kwa ujumla matatizo karibu yote yanatibika ni vyema kufika hospitali na kujua sababu na kutibu." Anasema Dk. Kikumbi.

Ugumba kwa wanaume unaweza kutokana na mifumo ya maisha kama ulevi kupindukia, sigara, kutofanya mazoezi lakini pia kazi mfano za viwandani zinazotoa mionzi, pia kuna maradhi ya ngono.

"Wanaume wanakuwa wagumu kutafuta matibabu mfano utasikia nina UTI sugu, inawezekana ni maambukizo ya magonjwa ya zinaa. Lakini hayatibiwi yanafichwa," anaonya mtaalamu huyo.

Anawakumbusha kinababa kuwa kufanya tendo la ndoa na kufikia kileleni au kuwa na nguvu nyingi za kiume, siyo uwezo wa kumpa mwanamke ujauzito.

Inawezekana manii zinazotoka hazina vichwa, haziwezi kukimbia, kuelea wala hazina nguvu, hivyo wasijiamini kwa vile wanaweza kujamiiana, anaonya.

## KUPANDIKIZA MIMBA

Dk. Kikumbi anasema kliniki ya kuchunguza na kupandikiza mimba KCMC inafanyika Jumanne na Alhamisi na wastani wa wateja 20 wanachunguzwa, wakati wa kliniki.

Anasema ili kusaidia wateja wagumba KCMC hutoa huduma mbili upandikizaji mdogo na mkubwa, mdogo unahusisha kusafisha manii kuondoa seli za magonjwa na zilizo hitilafu kama zisizo na kasi na vichwa.

Baada ya kupata mbegu zenye sifa zinaingizwa kwenye kizazi kwa kutumia mrija, upandikizaji unaogharamu Shilingi milioni 1.5. Aidha, mteja hahitaji kulazwa, anaeleza.

Kadhalika, anasema upandikizaji mkubwa unahusisha mbegu za baba na mayai ya mama kupimwa na kupata sifa zinazostahili, huunganishwa na kuwekwa maabara kwa siku tano, kisha kuhamishiwa kwenye kizazi, mchakato ambao mama analazwa hospitalini, ukigharimu kati ya milioni 10 hadi 12.

Unaweza kupandikiza mimba mara ngapi? Ni swali analoulizwa Dk. Kikumbi, anayeeleza kuwa isizidi mara tatu au nne, kuepusha athari za kiafya kutokana na mchakato huo wa kisayansi.

Anashauri wanaume na wanawake kuchunguzwa hali za uzazi hospitalini ili kutiba tatizo la ugumba, unyanyasaji na unyanyapaa.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, KISHAPU

# Bwawa lililofunikwa Mwadui lilivyogeuka kisima cha fursa



Wanakijiji cha Mwang'olo wakifuatilia upandaji vifaranga vya samaki katika bwawa jipya baada ya lile la awali kufunikiwa na tope mwaka jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

MWAKA mmoja umetimia, ilikuwa Novemba 7, 2022 kingo za bwawa la kuhifadhia majitope katika mgodi wa almasi Mwadui uliopo wilayani Kishapu, Mkoa wa Shinyanga, zilibomoka na kusambaza tope kwenye makazi na kuleta madhara.

Wakazi wa vijiji viwili ambavyo vipo jirani na mgodi huo, kikiwamo cha Nyenze na Mwang'olo viliathirika baadhi ya nyumba kufunikwa, tope kuharibu mali, kufukia mashamba, visima vya maji na bwawa ambalo wananchi walikuwa wakilitumia kuvua samaki na kuendesha maisha yao lilifukiwa.

Baada ya kufukiwa na tope la Mwadui, shughuli za uvuvi kwa wananchi zimekoma hadi sasa.

Ofisa Uhusiano Mgodi, Benard Mihayo, anasema baada ya kumaliza kulipa fidia, wanachokifanya sasa ni kurudishia kila kitu ambacho kiliharibiwa na tope katika hali yake, ukiwamo ujenzi wa bwawa jipya na kuweka miundombinu ya kupandikiza vifaranga vya samaki.

Anasema baada ya ujenzi wa bwawa jipya kukamilika lenye urefu wa mita za ujazo 270, ambalo lipo Kijiji cha Mwang'olo, wamepandikiza vifaranga vya samaki 5,000 vya aina ya sato, ili wananchi warudi katika maisha yao ya kawaida na kuendelea na shughuli za uvuvi.

**ELIMU WATAKAYOFAIDI**

Mihayo anaeleza kuwa ujio wa bwawa hilo ni fursa kwa wanavijiji kiuchumi na kiuwekezaji maana watapata elimu za aina mbalimbali.

> “Wavuvi tunashukuru mgodi wa Mwadui kwa kujenga bwawa hili jipya, na sasa wamepandikiza vifaranga vya sato na matarajio yetu baada ya muda tutarudi kwenye uvuvi na kuinuka tena kiuchumi.

Anasema watafunzwa kutunza bwawa, mbinu za kupata mbegu au vifaranga, kujua mbegu bora, ili kuvuna mavuno bora.

Aidha, Mihayo anasema wataelimishwa kuhusu usafi wa ndani na nje, kuondoa majani ili kuepusha wadudu na viumbe wengine kama vyura, nyoka, na kenge kula au kudhuru samaki.

Kadhalika mafunzo ya chakula jinsi ya kuandaa, kulisha samaki vyakula mbalimbali kama pumba ya mahindi, mashudu ya pamba, au alizeti, soya, mabaki ya dagaa au ya chakula kama ugali na wali.

Aidha, watafahamu magonjwa mfano ya vimelea au bakteria, virusi, minyoo, au magonjwa yatokanyo na lishe duni.

Elimu nyingine ni kuvuna samaki kupata wa kutosha na faida yote hayo yakitegemea kuzingatia aina ya samaki, kasi ya kukua ubora wa chakula na ulinzi wa bwawa, anaongeza.

Anaamini kuwa iwapo watatumia ujuzi huo wanaweza kubadilisha maisha na kuwekeza nje na ndani ya vijiji vyao kwa kutumia mafunzo na elimu hiyo.

Laurent Fabiani ni miongoni mwa waathirika wa tope hilo ambaye alikuwa akijishughulisha na uvuvi katika bwawa la zamani kabla ya kufunikwa na tope, anasema kwa sasa maisha yake ni magumu kwa sababu kazi yake kubwa ilikuwa ni uvuvi lakini ni jambo lililotokea kwa ghafla na kuwaacha na mshangao.

Fabiani baba wa familia ya watoto tisa, anasema tangu aache shughuli za uvivu mwaka jana baada ya bwawa kufunikiwa na tope, ameamua kujikita kwenye kilimo, ambacho ni matatizo kwa vile hutegemea mvua, mazao hukomaa baada ya muda mrefu na kipato hupatikana baada ya mavuno, hali ambayo anasema imeendelea kusababisha maisha yake kuwa magumu na yenye usumbufu kwa watoto wake.

Anasema zamani kabla ya bwawa kufunikwa na tope, kila kukicha akiwa na wenzake walikuwa wakienda kuvua na kuuza kwa wateja wa aina mbalimbali kukidhi mahitaji ya familia yake lakini pia akiwa na uhakika wa mboga, lakini sasa pesa hizo zimepotea na kumfanya kuwa na maisha magumu.

“Wavuvi tunashukuru mgodi wa Mwadui kwa kujenga bwawa hili jipya, na sasa wamepandikiza vifaranga vya sato na matarajio yetu baada ya muda tutarudi kwenye uvuvi na kuinuka tena kiuchumi,” anasema Fabiani.

Perepetua Bundala mkazi wa Kijiji cha Mwang'olo, anasema wamekuwa wakila mboga za majani kila siku, kutokana na kukosa samaki, kitoweo ambacho walikuwa wamezoa kula kila wakati na kilio chao ni tope lililofunika bwawa.

“Sisi wanawake ndiyo walinzi wa familia mboga ikikosekana inabidi twende mashambani kutafuta mboga za majani, na zamani tulizoea kila siku tunakula samaki, lakini siku hizi ni mwendo wa mboga za majani tukibadili ni dagaa na maharage,” anasema Perepetua.

Ofisa Uvuvi wilayani Kishapu Moses Ng'winza, anawasihi wananchi kwamba wasije wakaanza kuvua samaki hao, kwani ndiyo kwanza wamepandikizwa mwezi huu, ambapo wanapaswa kusubiri hadi miezi sita ndipo watakuwa wakubwa na tayari kwa kuvuliwa.

“Samaki hawa bado wadogo na miezi sita ikifika hakuna kuanza kuwavua mpaka pale mtakapopewa maelekezo na serikali pamoja na elimu ya uvuvi, ili samaki hawa waendelee kuzaliana na kuwa uchumi endelevu kwenu,”anasema Ng'winza.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Fatma Mohamed, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya Joseph Mkude, anapongeza mgodi kwa kuendelea kutekeleza maagizo ya serikali, na kurudisha kila kitu ambacho wananchi walikipoteza.

Fatma, anawasihi wananchi walitunze bwawa hilo la ufugaji samaki, na kuacha pia kulima kando yake, ili wakue na kuendelea kuzaliana, ambao watawainua kiuchumi na hata kuanza kuuza katika masoko makubwa, tofauti na zamani walikuwa wakiuziana kijijini kwao pekee.

“Nawasihi wananchi hii bahati msije ichezea, kila mmoja anapaswa kuwa mlinzi wa mwenzake kulilinda na kulitunza bwawa hili na samaki wake, na mtu atakayeonekana kulihujumu tupeni taarifa tutamchukulia hatua,” anaagiza Fatma.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwang'olo, William Burugu, anasema wananchi kwa sasa waaanza kupata matumaini ya kulea familia zao na kuinuka kiuchumi kupitia uvuvi wa samaki, na kueleza kwamba wataitisha mkutano wa hadhara kuzungumza na wananchi na kupewa elimu namna ya kulitunza bwawa hilo pamoja na kuweka ulinzi.

Anasema kila penye mafanikio hapakosi changamoto, kwamba wapo tu baadhi ya watu ambao ni wakorofi, hivyo ni lazima waliwekee ulinzi bwawa hilo ambalo limeshapandikizwa samaki ili kuwa mkombozi kwao kiuchumi.

Mwaka jana Novemba kingo za bwawa la kuhifadhia majitope katika mgodi wa almasi Mwadui lilibomoka na tope kuharibu mkazi na mali ya wananchi takribani 304 kutoka vijiji vya Nyenze na Mwang'olo ambao tayari wameshalipwa fidia za fedha ikiingizwa kwenye akauti zao ikifikia Shilingi bilioni 1.8.

Mbali na ulipwaji fidia hizo za fedha, wananchi ambao walipoteza thamani za ndani vikiwamo vitanda, magodoro, vyakula, majembe na pikipiki nao wamshalipwa fidia ya vitu hivyo, pamoja na waathirika 47 ambao walipoteza nyumba wameshajengewa nyumba zao na sasa wanasubiri kukabidhiwa.



## Wizara ya Elimu, SUA kushirikiana kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WIZARA ya Kilimo imeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) ili kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 hadi Bilioni tano ifikapo 2030.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hussein Omar, akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano hayo, alisema wamekubaliana ushirikiano kati ya Wizara na SUA ili kuhakikisha wizara inafikia malengo iliyojiwekea.

Alifafanua kuwa miongoni mwa makubaliano hayo ni kuzalisha wataalamu wa ugani watakaosaidia wakulima kuongeza uzalishaji utakaochangia mauzo ya mazao nje ya nchi na kuwakwamua kiuchumi wakulima.

Alibainisha kuwa ushirikiano huo utasaidia kufikia lengo la Wizara ya Kilimo kuongeza ajira milioni tatu kupitia kilimo ifikapo mwaka 2030.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo cha SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema wamejipanga kuhakikisha ufanikishwaji wa makubaliano hayo unafanyika kwa kiwango cha juu.

"Sisi kama chuo tuko tayari kwenda zaidi ya hiki tulichoandika katika ushirikiano wetu", alisema.

**Alibainisha kuwa ushirikiano huo utasaidia kufikia lengo la Wizara ya Kilimo kuongeza ajira milioni tatu kupitia kilimo ifikapo mwaka 2030.**

# Serikali kufanya utafiti kushuka viwango wahitimu elimu msingi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

SERIKALI imejipanga kufanya utafiti kwa ajili ya kuchunguza mwenendo wa kushuka kwa viwango vya wanafunzi kuhitimu elimu ya msingi na wanaojiunga elimu ya sekondari.

Ridhaa ya kufanya utafiti huo ilitolewa wakati wa mkutano wa mwaka wa Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo awamu ya Pili (EPforR II) ulioandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Utafiti huo utachunguza sababu kuu za kushuka kwa viwango hivyo na kupendekeza mikakati mahsusi na mbinu zinazofaa kushughulikia tatizo hilo.

Wakati huo huo, kulizinduliwa ripoti ya Novemba 2023 iliyotolewa na Programu ya Shule Bora inayolenga kuinua ubora wa elimu jumuishi kwenye mazingira salama ya kujifunzia kwa wasichana na wavulana katika shule za umma Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Msaada la Uingereza (UKAID).

Ripoti hiyo ilieleza kuwa Programu ya Shule Bora hivi karibuni ilishiriki kwenye kongamano la kimataifa la elimu lililofanyika Cambridge, Uingereza ambapo Naibu Katibu Mkuu (Elimu), Dk. Charles Msonde aliongoza wajumbe kutoka Tanzania ambao ni Dk. Anneth Komba, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE), Maofisa kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza (FCDO) na baadhi ya viongozi wakuu wa kiufundi wa programu ya Shule Bora.

Kongamano la Elimu na Maendeleo la Kimataifa la Uingereza UKFIET) ambalo hufanyika kila mwaka lilibeba mada inayosema elimu kwa haki ya jamii ya mazingira, utofauti, uendelevu, wajibu na kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa elimu, wakiwamo watendaji sekta ya elimu, watafiti, wawakilishi wa wafadhili na watoa elimu.

Wadau walishiriki kwenye mijadala muhimu kuhusu hali ya sasa ya elimu, athari zake, na ushawishi wake kwenye utungaji wa sera. Shule Bora iliwasilisha ubunifu wa kutoa motisha ya ugawaji wenye usawa wa walimu na zana za kufundishia kupitia Mpango wa Elimu wa Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR) Tanzania.

Aidha Timu ya Shule Bora pia ilipata fursa ya kutembelea Shule ya Sekondari ya OakGrove na Chuo Kikuu Huria cha Uingereza ili kutazama fursa ya kujenga ubia wenye malengo ya kuboresha ufundishaji wa lugha ya Kiingereza nchini Tanzania.

Aidha, ripoti hiyo imebainisha kuwa walimu 479 kutoka Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani wamenufaika na mbinu ya mafunzo ya jumuiya za ujifunzaji iliyotekelezwa kupitia programu ya Shule Bora kwa walimu 50 wa hisabati.

Chini ya uongozi wa Maofisa Elimu Kata na walimu wakuu, kila kata imejiwekea utaratibu wake wa kuhakikisha kwamba walimu wanakutana na kubadilishana ujuzi na maarifa muhimu.

Walimu 50 waliopatiwa mafunzo hayo walishirikishana na walimu wenzao ujuzi huo wa kufundisha aljebra, jiometri na vipimo na hivyo, kuwafikia jumla ya walimu 497 kupitia mbinu hii ambapo, mfano walimu 120 walifikiwa huko Kiluvya, 70 Kisarawe, 63 Msimbu, 45 Masaki na 19 wa Vikumburu.

Tathmini ya awali na baada ya mafunzo iliyofanywa kwa walimu hao ilionesha kuwa kuna ongezeko la umahiri kutoka asilimia 60.54 hadi kufikia asilimia 66.5.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikata utepe kuzindua Awamu ya Nne ya Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa baada ya kuzungumza katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa yaliyofanyika Nyerere Square jijini Dodoma juzi. Kulia kwake ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene na kushoto kwake ni Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Malecela asisitiza umuhimu wa elimu kwa kila Mtanzania

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, John Malecela, amesema kuwa kwa ulimwengu wa sasa ni lazima kila Mtanzania kuwa na elimu kwa ajili ya kujipatia maendeleo yake ya kiuchumi na kiroho.

Malecela aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye hafla ya kutunukiwa Shahada ya kwanza ya Theologia na Maendeleo ya Jamii aliyetunukiwa Askofu Mkuu wa Kansa la Covenant Faith Church Tanzania (Baba wa Matendo) Damas Thadey aliyeipata kutoka Chuo cha Rhema Bible Training College USA/Tanzania.

Mwanasiasa huyo mkongwe alisema kuwa kwa ulimwengu wa sasa kila Mtanzania anatakiwa kuwa na elimu bora ikiwemo ya kijamii na kiroho ambayo itamwezesha kufanya mambo ya maendeleo badala ya kuwa na elimu ya ubabaishaji.

Alisema kuwa iwapo watu watajikita kuwa na elimu bora itawezesha kufanya mambo ya kimaendeleo na kila watakachokifanya kuwa watafanya kwa uweledi wa hali ya juu kuliko mtu ambaye hana elimu ya kutosha.

Alibainisha kuwa hata watumishi wa Mungu kwa maana ya viongozi wa madhehebu ya dini wasiishie kwenye kutoa huduma ya kiroho tu bali pia wanatakiwa kuwa na elimu ya juu ambayo itawawezesha kuwa na uelewa wa mambo mbalimbali ya kijamii.

Alisema kuwa iwapo viongozi watakuwa wamepata elimu ni wazi kuwa watakuwa chachu ya kuwafanya watu wengine kupata elimu ambayo itawasaidia kuwaondolea ujinga na umaskini na kuwafanya waishi maisha ambayo kimsingi yanakubalika kwa viwango vinavyostahili.

"Mtu mwenye elimu tayari anakuwa ameshaondoa ujinga na umaskini kwani kila atakachokifanya kitakuwa na faida zaidi kwa manufaa yake na jamii inayomzunguka kwani mawazo yake yana upeo mkubwa wa kutambua ni wapi kuna fursa ya kumwezesha kujikwamua kimaisha.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Covenant Faith Church Tanzania Damas Thadey, aliwaomba viongozi wa madhehebu ya dini kuonyesha mfano kwa kuhamasisha waumini kujiendeleza kielimu zaidi ili waweze kupata uelewa na maarifa.

Thadey alisema kuwa viongozi wakionyesha mifano katika maendeleo taifa linaweza kuwa na faida kwa kuwa watu wake walio wengi watakuwa wasomi na wabunifu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kiroho.





# Wazazi wanyooshewa kidole ongezeko matukio ya ulawiti, mimba za utotoni

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

VITENDO vya ukatili hasa ulawiti na mimba kwa wanafunzi vimetajwa kuongezeka katika Halmashauri ya Mji Makambako Wilaya ya Njombe, huku sababu ikitajwa kuwa ni wazazi kutokuwa karibu na watoto wao.

Hayo yalielezwa na Ofisa Ustawi Jamii Halmashauri ya Mji wa Makambako, Masinde Masinde, wakati akizungumza na wazazi wa wanafunzi wa Shule ya Msingi za Mwembetogwa A, Azimio na Shule ya Sekondari ya Mukilima mjini hapa. Alisema asilimia 90 ya matukio ya ukatili yanagunduliwa na walimu na kueleza kuwa hiyo ni ishara ya kuwa wazazi hawapo karibu na watoto wao.

"Wazazi mtambue majukumu yenu, mnajisahau, nyinyi mnafikiri mkimpa mtoto huduma mmemaliza sasa mnampa kazi mwalimu, kinamama nyinyi mnayo nafasi pekee ya malezi na nyie wababa dunia sasa hivi imebadilika usiogope kuongea na mtoto wako," alisema Masinde.

Masinde, alisema kwa Kata ya Majengo pekee wamepokea kesi zaidi ya tatu za ulawiti kwa kipindi cha miezi mitatu huku wanafunzi watatu wa Mukilima Sekondari wamepata ujauzito kwa kipindi cha miezi miwili.

"Na shule hii ya Mukilima kuna mimba tatu tena wanafunzi walikuja kwa mpigo watatu, mmoja mara ya kwanza alishakuwa na kesi alilala kwa mwanaume shida ni wazazi hatuzungumzi nao, kaa zungumza na mwanao mjengee ujasiri," alisema Masinde.

Ofisa wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia na Watoto Makambako, Nsajigwa Andondile, aliwataka wazazi kutenga muda wa kuzungumza na watoto wao ili kubaini changamoto zinazowakabili.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Mukilima, Grasiano Sanga, alisema changamoto za kimalezi zimechangia kwa kiasi kikubwa kushuka kwa taaluma kwa wanafunzi.

Mmoja wa wazazi Nichoraus Nzaligo, alikiri kutumia muda mwingi kwenye shughuli za kiuchumi badala ya kukaa na kuzungumza na watoto na kueleza kuwa migogoro ya ndoa pia inachangia watoto kufanyiwa ukatili.




Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko, akiongea katika hafla ya kufunga maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya Shule ya Sekondari Nyamongo wilayani Tarime jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakiri kuwaficha watoto wenye ulemavu wakiogopa kuchekwa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

BAADHI ya wananchi wa Mtaa wa Idofi Halmashauri ya Makambako, mkoani Njombe, wamekiri kuwapo kwa changamoto ya baadhi ya wazazi kuwaficha na kuwafungia ndani watoto wenye ulemavu badala ya kuwaendeleza kielimu.

Wakizungumza na Nipashe katika halfa ya watoto wenye mahitaji maalumu ambayo ilifanyika Shule ya Msingi Idofi wananchi hao, walisema sababu kubwa ya kuwaficha watoto hao ni kuhofia kuchekwa ama kudharauliwa katika jamii kwa kuamini kuwa na mtoto mwenye ulemavu ni kama laana.

Mmoja wa wananchi hao, Maria Kinyunyu alisema ni baadhi ya wazazi wenye watoto hao kuwapeleka kanisani au kwenye vituo vya kulelea watoto na kuwatelekeza bila ya msaada wowote.

"Wengine wanaficha ndani wanasema mtoto huyu aoni mlemavu, yeye anamfungia tu ndani mwingine anazaliwa na kichwa kikubwa yaani mzazi anaona kama amekosea kumbe ni Mungu amempa," alisema Kinyunyu.

Naye Cosmas Sambala alisema kuwa tabia inayofanywa na baadhi ya wazazi ya kuwaficha watoto ndani sio nzuri kwa sababu hawakupenda kuzaliwa hivyo.

"Niombe wazazi wenzangu waweze kuwapeleka watoto shule ili wapate elimu kwa sababu na wenye ulemavu wanayo haki ya kusoma," alisema Sambala.

Awali Ofisa Elimu Maalumu Msingi na Awali katika Halmashauri ya Mji wa Makambako, Exavelia Mtega, alisema moja ya changamoto inayoikabili shule hiyo ni uhaba wa bajeti ya chakula kwa wanafunzi wenye uhitaji maalumu kwani serikali inatoa chakula cha wanafunzi 22 pekee lakini wanafunzi waliopo ni 65.

"Shule hii pia inakabiliwa na uhaba wa walimu wa kufundisha wanafunzi wenye uhitaji maalum, pamoja na kukosekana kwa bima za afya kwa wanafunzi wote wa vitengo na jumuiya," alisema Mtega.

Kaimu Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Mji Makambako, Yusto Nyamle, alitoa rai kwa wazazi kuhakikisha wanaandikisha watoto wao ili wajiunge darasa la kwanza mwakani.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Mahongole, Mario Kihombo, alisihi wazazi kuacha dhana potofu juu ya watoto wenye ulemavu na kusema kuwa Baraza la Madiwani litahakikisha serikali inatatua changamoto ya upungufu wa chakula kwa halmashauri kutenga bajeti.

"Kwa yeyote mwenye mtoto nyumbani haruhusiwi kumuacha eti kwa sababu hatembei, eti kwa sababu haoni, eti kwa sababu hasikii, ulemavu wa aina yeyote utakiwa kumleta shule ili aweze kupata kipaji chake," alisema Kihombo.

Kihombo alisema ipo haja ya halmashauri kupitia mapato ya ndani kutenga bajeti ya kusaidia kutatua changamoto kwenye shule zenye uhitaji maalum.

# Wakulima parachichi waomba bei elekezi

**NA Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa parachichi Wilaya ya Njombe, mkoani Njombe wameiomba serikali kuweka bei elekezi ya zao hilo sambamba kuwaunganisha na masoko ya moja kwa moja ili kuwadhibiti madalali.

Wamesema zipo kampuni za kinyonyaji zinazokwenda mashambani kwa wakulima na kununua parachichi kwa bei ndogo zaidi ili kujitengenezea faida kubwa hatua ambayo inawafanya wakulima kukosa fedha za kuhudumia mashamba.

Changamoto hizo walizitaja baada ya kutembelewa kwenye mashamba yao katika Kijiji cha Matembwe wilayani Njombe na Muungano wa Wakulima wa Miti Tanzania TTGAU pamoja na maofisa wa Shirika la Chakula Duniani FAO.

Mkulima Batweli Peter alisema licha ya zao hilo kuvutia wawekezaji wengi na kubadili maisha ya jamii nyingi za wakulima shida kubwa inayokwamisha kupiga hatua ni unyonyaji unaofanywa na madalali na kampuni kandamizi.

Alisema ili kukomesha unyonyaji huo ni vyema serikali ikaunda vyama vya wakulima wa parachichi na kuwaunganisha masoko ya moja kwa moja na kuwajengea wakulima mifumo ya umwagiliaji ili kuongeza kiwango cha mazao yenye tija sokoni.

"Wale wanakuja bila ya kujua mkulima amegharamia kiasi gani, yeye anakuja tu na bei zake zile ambazo na yeye anataka apate kwa hiyo wanatuyumbisha kwenye bei," alisema Peter.

Laurent Mfugale alisema kwa sasa hakuna soko la zao hilo na likipatikana wanauza kwa bei wanazotaka madalali jambo ambalo halina faida kwa mkulima ukilinganisha na gharama za uendeshaji.

Mkurugenzi wa TTGAU, Castory Timbula alisema mafanikio wanayoyapata hivi sasa wakulima ni kutokana na mfunzo waliowajengea kupitia mradi wa FFF unaofadhiliwa na Shirika la Chakula FAO wenye lengo la kutunza mazingira na kuwaongezea kipato.

Naye Mratibu wa mradi wa FFF, Godfrey Bakanga, alisema ili mradi huo ulete mageuzi kwa wakulima wa parachichi ni lazima kuunda vikundi kote nchi ambavyo vitakuwa na sauti ya kupanga bei ya pamoja.

"Mradi umekuwa ukisaidia katika mwelekeo wa vikundi na wabaki kwenye mwelekeo huo maana yake hata bei ya soko waijadili kubaki na sauti moja kama kikundi isiwe mtu mmoja mmoja, mtu mmoja atakuja dalali atampa kwa bei ya chini ataharibu soko," Bakanga alisema.





# Rais Mwinyi mgeni rasmi Siku ya Maadili na Haki za Binadamu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR



RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi anatarajiwa kuwa mgeni katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yatakayofanyika leo visiwani Zanzibar katika Ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Kikwajuni.

Akizungumza jana na waandishi wa habari Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema maadhimisho hayo yanatokana na tamko la kimataifa lililoidhinishwa mwaka 2003 na siku ya haki za binadamu duniani ambayo hufanyika Desemba 10 ya kila mwaka.

Alisema tamko la kimataifa liliidhinishwa na kupitiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1948, hivyo serikali zote mbili nchini Tanzania zimekubaliana kuadhimisha siku ya maadhili na haki za binadamu kimataifa.

Waziri Haroun alisema tangu Zanzibar kuadhimisha siku hiyo mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kuongezeka kwa uadilifu kwa viongozi katika kufanya majukumu yao.

Waziri huyo alisema katika kufikia maendeleo ya Zanzibar lazima wananchi wana wajibu katika kutoa maoni juu ya mambo mbalimbali na huo ndiyo utawala bora na haki za binadamu.

Alisema wizara imefanya kazi kubwa kuwaelimisha wananchi kutambua wajibu wao hasa katika haki za binadamu. Kauli mbiu katika maadhimisho hayo ni tuimarishe utawala bora na haki za binadamu kwa kuondoa ubadhirifu na kukuza maadili kwa ustawi wa jamii.

# Taasisi za Kiswahili zaagizwa kuongeza kasi ya ufundishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema lugha ya Kiswahili inamchango mkubwa katika kukuza diplomasia ya uchumi hivyo ni wajibu kwa taasisi zinazofundisha lugha hiyo kuongeza kasi ya kuikuza na kuieneza duniani.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema hayo jana wakati akifungua kongamano la saba la Kiswahili la Kimataifa lililofanyika katika ukumbi wa Shekh Idrisa Abdulwakili Kikwajuni Zanzibar.

Alisema katika kukabiliana na hatua hiyo ni jambo la msingi kuongeza programu za ufundishaji kwa walimu wa ndani na nje kuifundisha lugha hiyo katika maeneo mbalimbali ili kuongeza mapato na kukuza uchumi wa nchi.

Waziri Tabia alisema lugha hiyo moja ya zinazotumika Afrika na inasaidia kusukuma mbele ajenda ya Afrika Mashariki ambayo ni moja ya kipaumbele cha uchumi wa Afrika na duniani kote.

Alisema katika kuthamini lugha hiyo, sasa hivi kuna mwamko mkubwa kwa wanafunzi kujifunza katika vyuo vikuu na vya ualimu kutokana na kupewa kipaumbele kikubwa duniani.

Tabia alitumia fursa hiyo kuwataka washiriki wa kongamano hilo kulitumia ipasavyo ili iwe kichocheo cha bidhaa bora zinazosambaza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu katika shughuli mbalimbali.

Hata hivyo aliwataka waandaaji wa kongamano hilo kuhakikisha wanatanua wigo ili kongamano lijalo kuwafikia wataalamu kutoka nchi mbalimbali ili kutoa michango yao juu ya kuikuza zaidi lugha hiyo.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Hamad Rajab alisema lugha hiyo hivi sasa imekuwa kutokana na baadhi ya wageni kununua kamusi za Kiswahili na kwenda kufundisha ndani ya nchi zao.

Alisema hatua hiyo imesaidia kukifanya Kiswahili kupiga hatua kubwa ya kimaendeleo kwa mustakabali mwema wa nchi na taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Baraza la Kiswahili, Dk. Saade Said Mbarouk, alisema baraza linaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa lugha ya Kiswahili ili kuwafundisha wageni kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kueneza lugha hiyo duniani.

Akiwasilisha makala elekezi juu ya Kiswahili na diplomasia duniani Suleiman Hukum Said alisema lugha ya kiswahili ina wazungumzaji zaidi ya milioni 200 dunia nzima kutokana na jitihada zinazofanywa na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA).

Akichangia katika kongamano hilo Mhadhiri Msaidizi Kutoka Chuo cha Catholic Mbeya (CUCoM, Sebastian Nyerere Mbwillow, alisema kuwepo kwa vilabu vya wanafunzi katika vyuo vikuu vinavyozungumza kiswahili itakuwa chachu ya kukuza maendeleo ya lugha hiyo.

Alisema katika kukuza lugha hiyo pia kuna haja ya kutoa kipaumbele kwa wataalamu wa lugha ya alama ili iweze kuwafikiwa watu mbalimbali ikiwamo wenye mahitaji maalum.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (wa pili kushoto), akimkabidhi tuzo ya shukrani Mkuu wa Kitengo cha Bima wa Benki ya NMB, Martin Massawe (wa tatu kulia), kwenye hafla ya Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa Mwaka 2022 iliyofanyika jijini Dar es Salaam. Kutoka kulia ni Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware, Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Balozi wa Bima, Zena Saidi na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Bima, Moremi Marwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uhaba wa ajira chanzo wasomi kutorejea Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Zanzibar, Ali Abdulgulam Hussein, amesema kuchelewa kupatikana ajira kwa wataalamu waliokwenda kusoma nje ya nchi ni miongoni mwa sababu baadhi yao kushindwa kurudi au kutafuta ajira sehemu nyingine ikiwamo Tanzania Bara.

Gulam alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdalla Ameir, aliyehoji sababu za baadhi ya wataalamu wanapomaliza masomo yao kutafuta ajira nyingine au wengine kubaki nje ya nchi.

**Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mkazo wa kutoa ajira kwa fani za sekta ya afya ikiwamo madaktari bingwa kutokana na mahitaji yake makubwa.**

Alisema wataalamu wanaporudi nje ya nchi wizara husika huandika barua kwenda utumishi kuwajulisha kuhusu kumaliza masomo kwa mwanafunzi husika kwa ajili ya kupatiwa ajira.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mkazo wa kutoa ajira kwa fani za sekta ya afya ikiwamo madaktari bingwa kutokana na mahitaji yake makubwa.

Aidha alisema Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inahakikisha wanafunzi wote wanaokwenda nje ya nchi kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu wanarudi nchi mara wanapomaliza masomo yao kwa ajili ya ajira na kulipa mikopo wanayodaiwa.

Naibu huyo alisema jumla ya wanafunzi 1,177 wamepatiwa udhamini wa masomo ya elimu ya juu katika fani ya udaktari katika vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kuanzia mwaka 2019-2023.

Alisema matarajio ya serikali ni kuona wanafunzi wote wanaokwenda kusoma nje ya nchi mara wanapomaliza wanarudi nchini kwa ajili ya kuanza utumishi wa serikali pamoja na kulipa mikopo ya elimu ya juu.

"Hayo ndiyo matarajio yetu kuona wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi wakipata ufadhili wa serikali wanarudi nchini na kufanya kazi pamoja na kulipa mikopo ya elimu ya juu," alisema Gulam.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA VYETI



**MARIAMU PETRO NG'ENI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye Index No. S1861/0012/2017 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MERYA SECONDARY SCHOOL mwaka 2017, Cheti cha kidato cha sita chenye No. S0281/0654/2020 kilichotelewa na CHIEF IHUNYO GIRLS HIGH SCHOOL mwaka 2020. Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/11137/2023**
Taarifa ya polisi: **PHQ/DOD/DOD/11135/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 7 YA MWAKA 2023**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**APAEL HEZRON NGURE............MAREHEMU**
**EBENEZER H. NGURE..............MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa Muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 18 Mwezi wa Disemba, Mwaka 2023.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 20 Mwezi wa Novemba Mwaka 2023.

Principal Resident Magistrate
Mwanga

---

**WIZARA YA ARDHI,NYUMBA NA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MASWA.**
**LILILOPO MASWA.**
**MAOMBI MAKUBWA NA.58 YA MWAKA 2023**
**KATI YA**
**HUMU MAHU PUNDU.............MLETA MAOMBI**
**(Msimamizi wa mirathi ya Marehemu Mahu Pundu Ng'humbe)**
**DHIDI YA**
**PENDO NG'HABI..............................Mjibu Maombi**
**MBALU MSOMA.............................Mjibu Maombi**

**WITO/TAARIFA**

**Kwa: MBALU MSOMA POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yako na wenzako katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya madai yanaweza kupatika hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 14.12.2023.
Pia unajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 14.12.2023 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.
Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.
IMETOLEWA kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza hili leo tarehe 30.11.2023

**J.T.KAARE**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA(W)**
**MASWA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Maswa Kituo cha NYABUBINZA Mkoa SIMIYU**

**Shauri la Madai No.16 2023**

**Jina la Mdai NGONYIWA NKOBA MATABA**

**Jina la Mdaiwa SHILINDE BUKOYE MATABA.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama ya Mwanzo kwa SHIKINDE BUKOYE MATABA

Mkazi wa kitongoji cha Bukingwaminzi Kijiji cha Shishiyu Kata ya Shishiyu Wilayani Maswa Mkoani Simiyu.

**K.K VEO-SHISHIYU**
**MASWA**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba madai yake ni **(Sh.2,500,000/) tu Million mbili na laki tano tu**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 13 Mwezi 12 Mwaka 2023 Saa 02:30 asubuhi kwa mujibu wa Madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hii ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hii kwa ajili ya kujitetea

**ANGALIZO:** kama hutohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 Mwezi 11 Mwaka 2023.

MAHAKAMA YA MWANZO NYABUBINZA MASWA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYABUBINZA

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA HANDENI**
**MAOMBI NA...43...............MWAKA ....2023**
**RIZAO ABDALLAH .........................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**GODFREY VICTOR NYANGE ...................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: .......GODFREY VICTOR NYANGE ...C/o ...WEO KATA YA KIDELEKO.**

Fahamu Kwamba shauri hili limepangwa kutajwa desemba 12, 2023 saa 8:30 asubuhi mbele ya
Mh. Ngonyani K.C, Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Unatakiwa kufika wewe mwenyewe au wakili wako pasipo kukosa.
Amri hii inatolewa kwa mkono wangu na lakiri/ muhuri wa Baraza hili leo 14/11/2023.

.............................................
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA.**
**HANDENI.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HATIBU HASSANI ATHUMANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 932 CAC.** Chassis namba **LTBPK8BG912K02985.** Engine namba **KL162FMJ18J02985.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/1407/2023.**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**

**MISC. CIVIL APPLICATION No. 09 of 2023**
**(Original from Civil Case No. 02 of 2023)**

**EVARISTA NJILEKIRO KALALU......APPLICANT**

**VERSUS**

**SALAGO KISABO @ KIJA..............RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE FOR HEARING**

**TAKE NOTICE THAT,** the above case has been fixed for Hearing on the 08th day of January, 2024 at 08:00 am.
**YOU ARE** required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**GIVEN** under my **HAND** and the **SEAL** of the Court this 11th day of December, 2023.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO, KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......121/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ALDO CHESAM wa TUNGI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA MIKIDADI CHESAM**

**TANGAZO**
***(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 12 mwaka 2023

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI kituo**
**Cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 96/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ELIZABETH ERASTO MSEMNE WA IPAGALA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA RICHARD JOSHUA KAMUNYA**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 08 Mwezi 12 Mwaka 2023

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA Kituo cha MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 127/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SALEHE SAIDI ATHUMANI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MOHAMED SALEHE SAID**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 05 Mwezi 12 Mwaka 2023

---




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Vifaa vya uchaguzi vyawasili DRC

**KINSHASA,** DRC

TUME Huru ya Uchaguzi (CENI) nchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) imesema vifaa vyote vya uchaguzi vilivyoagizwa kutoka China tayari vimewasili na kuthibitisha kufanyika kwa uchaguzi mkuu Desemba 20, mwaka huu.

Mmoja wa wasemaji wa CENI, Jean-Claude Munganga, alisema tume hiyo ilipokea zaidi ya kilo 92,000 za vifaa vya uchaguzi mwishoni mwa wiki ambavyo ni mzigo wa mwisho unaojumuisha hati nyeti pamoja na karatasi za matokeo na zile za maelezo kuhusu uchaguzi.

**Tuko wakati wa kampeni za uchaguzi katika nchi kubwa ambako ndege ndiyo njia pekee ya kupitia ili kufika katika mikoa.**

"Tarehe 20 kutakuwa na uchaguzi kwa sababu vifaa vyote kwa ujumla vipo tayari na kweli vimesambazwa. Vifaa hivyo kwa mfano ni karatasi za matokeo, karatasi za maelezo, wino usiofutika, vyeti vya kura, yaani karatasi zote zipo na vifaa tayari viko hapa," alisema Munganga.

Aidha, ilielezwa kuwa wakati uchaguzi huo ukithibitishwa, baadhi ya wagombea urais hawana tena jinsi ya kuendelea na ziara mikoani. Na kwamba wamekwama kutokana na ukosefu wa mafuta ya ndege.

Kutokana na hali hiyo inaelezwa kuwa wanaulaumu utawala wa Rais Félix Tshisekedi kwa kuzuia mafuta katika kila uwanja ili kuwakwamisha wapinzani.

Miongoni mwa waliokumbwa na kadhia hiyo ni mgombea Martin Fayulu aliyekwama mkoani Equateur wakati akisubiriwa huko Lubumbashi.

Katibu mkuu wa chama cha siasa cha Fayulu, Devos Kitoko, alisema "Tuko wakati wa kampeni za uchaguzi katika nchi kubwa ambako ndege ndiyo njia pekee ya kupitia ili kufika katika mikoa. Lakini serikali ya nchi inayojiita Jamhuri ya Kidemokrasia inazuia ndege za kibinafsi kununua mafuta. Kwa hiyo nalaani vitendo hivyo visivyo vya kidemokrasia".

Mgombea Dénis Mukwege pia alitoa malalamiko hayo hayo akiilaumu serikali kwa kuzuia upatikanaji wa mafuta.

Malalamiko hayo yanatolewa chini ya siku kumi kabla ya uchaguzi mkuu ambao Wakongo watamchagua Rais wa Jamhuri, wabunge wa kitaifa na wale wa mikoa, pamoja na washauri wa manispaa. **DW**



Wapigakura nchini DRC wakiangalia majina yao kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Desemba 20, mwaka huu. **PICHA MTANDAO**

## Zelenskyy kukutana na Joe Biden leo

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS Joe Biden atakuwa mwenyeji wa Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskyy huko White House leo wakati utawala wa Marekani ukiongeza msukumo wake kwa bunge kuidhinisha msaada wa ziada kwa Ukraine katika vita vyake vya kujihami dhidi ya Russia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na White House ziara hiyo ya Rais Zelenskyy inalenga kusisitiza dhamira ya Marekani ya kuwasaidia watu wa Ukraine wakati wakijitetea dhidi ya uvamizi wa Russia.

Ofisi ya Zelenskyy ilithibitisha kuwa amekubali mwaliko wa Biden. Pia alialikwa kuzungumza kwenye mkutano wa maseneta wote.

Ilielezwa kuwa Rais Biden anawaomba wabunge katika Bunge la Marekani kutoa dola bilioni 110 za mfuko wa fedha wa vita kwa Ukraine (dola bilioni 61.4) na Israel, pamoja na vipaumbele vingine vya usalama wa taifa.

Aidha, ilielezwa kuwa Warepublican katika bunge la seneti la Marekani walizuia mswaada huo, wakisema mabadiliko makubwa ya usalama wa mpaka wa Marekani yalihitajika. **VOA**


Joe Biden


Volodymyr Zelenskyy

## UN yasisitizwa kuongeza uwezo wa misaada Gaza

**TEL AVIV,** Israel

BODI ya Wizara ya Ulinzi ya Israel inayosimamia sera kwa maeneo ya Palestina, (COGAT), imesema Umoja wa Mataifa (UN) lazima ufanye vyema zaidi katika kupeleka misaada kwa watu huko Ukanda wa Gaza.

Chapisho kwenye mtandao wa X, zamani Twitter, lililowekwa jana lilisema Israel imepanua uwezo wake wa kukagua misaada inayotolewa kupitia kivuko cha mpaka cha Rafah kinachodhibitiwa na Misri, na kwamba kivuko cha bidhaa cha Kerem Shalom kinachodhibitiwa na Israel kitafunguliwa kwa mara ya kwanza tangu vita vilipoanza.

"Msaada unaendelea kusubiri kwenye lango la Rafah. Umoja wa Mataifa lazima ufanye vyema zaidi, misaada ipo na watu wanaihitaji," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Katika muhtasari wake wa hivi karibuni, ofisi ya Umoja wa Mataifa ya masuala ya kibinadamu inasema uwezo wa wafanyakazi wake huko Gaza kupokea misaada inayokuja umeharibika kwa kiasi kikubwa katika siku chache zilizopita kutokana na mambo kadhaa.

"Hizi ni pamoja na uhaba wa malori ndani ya Gaza, kukatika kwa mawasiliano ya simu, na kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi ambao hawakuweza kusafiri kwenda kwenye kivuko cha Rafah kutokana na uhasama mkubwa," ilisema.

Umoja wa Mataifa pia unasema usambazaji wa misaada pia umesimama kwa kiasi kikubwa nje ya eneo la Rafah katika siku chache zilizopita kutokana na mapigano makali na vikwazo vya kutembea kwenye barabara kuu, hasa ndani na karibu na mji wa karibu wa Khan Younis. **BBC**

## UN kuondoa majeshi Mali

**BAMAKO,** Mali

MSEMAJI wa Umoja wa Mataifa (UN) Fatoumata Kaba, amebainisha kuwa ujumbe wa walinda amani wa umoja huo nchini Mali umemaliza muda wake baada ya kuhudumu kwa kipindi cha miaka 10.

Kwa mujibu wa taarifa ya UN, hatua hiyo imekuja baada ya utawala wa kijeshi nchini humo kutaka Umoja wa Mataifa kuwaondoa walinda amani wake.

Kaba alisema ujumbe huo ambao unafahamika kama MINUSMA, umeshusha bendera za Umoja wa Mataifa katika makao makuu yake jijini Bamako.

"Tukio hilo linaashiria kumalizika rasmi kwa muda wa ujumbe huo japokuwa baadhi ya maofisa wake wangali kwenye taifa hilo," alisema Kaba.

Utawala wa kijeshi nchini Mali ambao ulichukua madaraka Juni 2020, ulitoa wito kwa UN kuwaondoa wanajeshi wake katika ardhi yake ambao walitumwa huko mwaka wa 2020 kwa lengo la kudumisha amani.

Aidha, ilielezwa kuwa hatua ya kuondoka kwa wanajeshi hao inakuja licha ya nchi hiyo ya Sahel kuendelea kukabiliwa na tishio la makundi yenye silaha.

Hata hivyo ilibainishwa kuwa kumekuwapo na hofu kuwa kuondoka kwa wanajeshi wa UN, kutasababisha kuongeza kwa makabiliano ya kudhibiti baadhi ya maeneo kati ya wanajeshi na makundi ya watu wenye silaha.

MINUSMA ilikuwa na maofisa wa usalama karibia 15,000 nchini Mali ambao karibia 180 wameuawa wakiwa kazini katika mazingira hatari.

Vile vile inaelezwa kuwa tangu watakiwe kuondoka, walinda usalama wa MINUSMA wameondoka katika maeneo 13 nchini Mali na wanatarajiwa kufunga kambi zao katika mji wa Gao na Timbuktu kaskazini mwa taifa hilo.

Juma lililopita, ujumbe huo wa UN ulikabidhiana kambi ya Mopti katikati mwa Mali kwa mamlaka mojawapo ya maeneo ambayo yanakabiliwa na utovu wa usalama kutoka kwa wanajihadi. **RFI**

# SIMBA QUEENS YAANIKA TATIZO YANGA PRINCESS

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Charles Haalubono, amekiri kukosa mshambuliaji halisi imekuwa tatizo kwenye timu yake kushindwa kufanya vizuri mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba Queens.

**Yanga Jumamosi walishindwa kusonga mbele kwenda kucheza fainali kutokana na kuondolewa kwenye hatua ya nusu fainali kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya kutoka suluhu ndani ya dakika 90 katika Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi Dar es Salaam.**

Baada ya mchezo huo, Kocha huyo wa Yanga Princess, Haalubono, alisema mechi ilikuwa nzuri na amependa ushindani kutoka kwa Simba Queens kwa sababu amekutana na timu nzuri na bora.

Alisema suala la penalti ni bahati ambayo haikuwa upande wao na walifanya kazi kubwa katika ukabaji kwa sababu waliwasoma vizuri Simba Queens, lakini kukosa mshambuliaji halisia ilikuwa tatizo kwao.

"Tumecheza vizuri na hatukuweza kutumia nafasi katika dakika 90 za mchezo licha ya kutengeneza nafasi nyingi, lakini tumekosa mshambuliaji halisia na kushindwa kufanya vizuri, hivyo tunaenda kujiandaa kwa mechi ya mshindi wa tatu," alisema Haalubono.

Naye Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wachezaji wao walipambana pia mabadiliko ya benchi la Simba kumewawezesha kuimarisha timu hiyo kuwa imara zaidi.

Pia alisema Yanga wamefanya mabadiliko nao kwenye benchi la ufundi na wamejitahidi kuonesha ubora na kuleta ushindani ndani ya dakika 90 kwa kucheza mpira mzuri.

"Tumefanikiwa kusonga mbele kwenda kucheza fainali, Yanga wamefanya 'sapraizi' hatukutegemea, hatukuwa na muda wa kujiandaa kwa sababu tumekua tunafanya maandalizi kimafungu kutokana na wachezaji wetu kuwapo kwenye majukumu ya kimataifa.

"Ukiangalia mfumo tulиocheza leo (Jumamosi) ni tofauti kwa sababu wachezaji waliokuwa mbele hawajawahi kufanya mazoezi pamoja," alisema kocha huyo msaidizi.

Aliongeza kuwa wameona mapungufu ya kikosi chao na wanaenda kufanyia kazi kwa ajili ya mchezo wa fainali dhidi ya JKT Queens na wamefanikiwa kuwaona wapinzani wao hao.

"JKT ya hivi sasa ndio asilia kwa hiyo fainali itakuwa nzuri, kuna nafasi ya kuchukua ubingwa wa Ngao ya Jamii na kurejesha ufalme wetu," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Simba.

Simba Queens itashuka Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam leo kumenyana na JKT Queens katika fainali ya Ngao ya Jamii kwa Wanawake ikiwa ni baada ya kuiadhibu Yanga Princess kwa mikwaju ya penalti 5-4 katika mchezo wa nusu fainali wakati JKT Queens yenyewe iliichapa Fountain Gate Princess mabao 5-0 na kutinga fainali.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga Princess kuwania nafasi ya tatu dhidi ya Fountain Gate Princess, mechi zote zikitarajiwa kuchezwa leo katika Uwanja wa Azam Complex.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Tigo Kanda ya Ziwa, Joseph Mutalemwa (kushoto), akimkabidhi mshindi wa Magift Dabodabo mfano wa hundi ya shilingi milioni tano, mkazi wa Kidinda mkoani Simiyu, Robin Brasio, alipomtembelea kwenye duka lake la spea za pikipiki eneo la Njiapanda ya Ngulyani mjini Bariadi mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mkazi Simiyu akabidhiwa 'Magift Dabodabo'*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Huduma za Mawasiliano ya Tigo, imekabidhi zawadi kiasi cha shilingi milioni tano kwa Robin Brasio wa mkoani Simiyu ambaye aliibuka mshindi wa Kampeni yao ya 'Magift Dabodabo.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika eneo la Njiapanda ya Ngulyati Simiyu, Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Ziwa, Joseph Mutalemwa, aliwakumbusha wakazi wa mkoani humo na nchi nzima kuchangamkia fursa ya kampeni hiyo ili waweze kushinda zawadi mbalimbali.

"Kampuni yetu inawajali na kuwapenda wateja wake, mnachotakiwa kufanya ni kufanya miamala na kujiunga na vifurushi kila wakati ili kubahatika kujishindia zawadi mbalimbali hata ile zawadi kubwa ya magari mawili, ambapo moja utampa umpendaye," alisema Mutalemwa.

Aidha, Diwani wa Kata ya Bariadi, Kija Bulenya, aliishukuru Tigo kwa kumpatia zawadi kijana wa Bariadi ambapo kwake imekuwa mara ya kwanza kushuhudia mshindi akipewa zawadi.

"Ni furaha ilioje kwangu kuona mkazi wa hapa Bariadi akipewa pesa alizoshinda, huwa nasikia tu matangazo ya Magift Dabodabo kwenye runinga na redio, nichukue fursa hii kuwahamasisha wakazi wa Bariadi na nchi nzima kuendelea kutumia huduma za Tigo kwa wingi," amesema Bulenya.

Kwa upande wa mshindi wa Magift Dabodabo, Robin Brasio, alisema hakuamini alipoambiwa ameshinda katika kampeni hiyo na kuishukuru Tigo.

"Pesa hii nitanunua bodaboda moja na kufanya biashara ili iniingizie kipato, pesa zitakazobaki nitaongeza spea za pikipiki hapa katika duka langu ili niuze na kupata faida," alisema Brasio.

## Uhamiaji FC kuongeza nguvu dirisha dogo

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji FC imesema inaendelea na mipango yake ya kukiboresha kikosi chake ili kuweza kupata matokeo mazuri kwenye Ligi Kuu Zanzibar inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Uhamiaji FC, juzi ilitoka sare ya bila kufungana dhidi ya Maafande wa Mafunzo SC katika mwendelezo wa ligi hiyo ikiwa ni mchezo wa mwisho wa mzunguko wa 14, ambao ulichezwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa 10 alasiri, matokeo ambayo yanaifanya hadi sasa kukusanya jumla ya pointi 18 katika nafasi ya saba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdu-salehe Abdallah, alisema awali timu hiyo ilifanya maandalizi yake mazuri, lakini kutokana na ushindani uliopo katika ligi hiyo kwa sasa, bado anadhani maboresho yanahitajika ili kuwa na kikosi bora utakapoanza mzunguko wa lala salama.

Alisema ingawa hawapo katika nafasi ya hatari zaidi, lakini wanahitaji kupata alama tatu hasa katika michezo yake ya nyumbani ili kujiweka katika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Mapumziko ya dirisha dogo tunatakiwa kuyatumia vizuri kwa kukiboresha kikosi chetu katika nafasi zote ambazo tunaomba zinamapungufu, hii itatufanya mzunguko wa lala salama tuwe bora zaidi na kuhakikisha kwanza michezo ya nyumbani tunapata alama tatu," alisema.

## Singida kusaidia waathirika wa mafuriko Hanang

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Singida Fountain Gate umesema mapato waliyoyapata katika mchezo wao waliocheza jana dhidi ya KMC watayapeleka kwa waathirika wa mafuriko yaliyotokea katika wilayani Hanang mkoani Manyara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema wameamua kutoa mapato hayo ili kuiunga mkono Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jitihada za kuwasaidia waathirika hao wa mafuriko.

Alisema wamepotea Watanzania wengi katika mafuriko hayo, hivyo kuwataka Watanzania kuendelea kuwasaidia wale wote walioathirika kwa nyumba zao kusombwa na mafuriko pamoja na walioopoteza ndugu zao.

Katika hatua nyingine Masanza alikiri ligi msimu huu ina ushindani kwani kila timu inataka ishike nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

## ZISIKUPITE

### VARANE KUKIMBIZWA

RAPHAEL Varane huenda akaondoka Manchester United Januari kwa vile beki huyo wa zamani wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 30, hana uhusiano mzuri na Kocha Erik ten Hag. ***(Nicolo Schira)***

### SAMUELE ANUKIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inaongoza katika mbio za kumsajili winga Mwingereza Samuel Iling-Junior kutoka Juventus, mwenye umri wa miaka 20. ***(Football Insider)***

### SANGANTE AWINDWA FULHAM

KLABU ya Fulham inaimarisha mpango wake wa kumnunua kiungo wa Le Havre raia wa Senegal, Arouna Sangante, 21. ***(Sun)***

### ANDRE KUTIMKA FLUMINENSE

FULHAM pia imeonesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Fluminense raia wa Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22. ***(Nicolo Schira)***

### BERGKAMP KUREJEA ARSENAL

KOCHA Mikel Arteta amemwalika gwiji wa Arsenal, Dennis Bergkamp, kurejea katika klabu kama sehemu ya wakufunzi wa chuo chao cha soka. ***(Football transfers)***

### BEIER KUONDOKA LIVER

LIVERPOOL ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu England zinazomtaka mshambuliaji wa Ujerumani, Maximilian Beier mwenye umri wa miaka 21, ambaye anatarajiwa kuondoka Hoffenheim msimu ujao. ***(Sky Sports)***

### GODFREY ASIKILIZIA SPURS

KLABU ya Everton iko tayari kumuuza beki wa England, Ben Godfrey mwenye umri wa miaka 25, kwa Tottenham Hotspur Januari iwapo dau litawasilishwa. ***(Football Insider)***

### ARAUJO AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imetoa ofa ya kumpa mshahara mnono zaidi beki wa Barcelona, Ronald Araujo, 24. ***(Mundo Deportivo)***

### TEL KUBAKI BAYERN

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Mathys Tel mwenye umri wa miaka 18, ameamua kubakia Bayern Munich hadi msimu ujao, licha ya klabu kadhaa kutaka kumsajili kwa mkopo, ikiwa ni pamoja na Manchester United. ***(Sky Sports Germany)***


### WILLIAN ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA imefanya mazungumzo na Palmeiras kuhusu dili la kumsajili winga wa Brazil, Estevao Willian mwenye umri wa miaka 16, anayejulikana kama 'Messinho', ambaye pia anavutiwa na Barcelona. ***(Goal, via Mundo Deportivo)***

### TODIBO ANYATIWA EPL

KLABU ya Manchester United ipo kwenye mbio moja na Tottenham Hotspur katika mbio za kuwania saini ya mlinzi wa Nice na Ufaransa, Jean-Clair Todibo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATAKA ZAIDI KUTOKA KWA WACHEZAJI

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amewataka wachezaji wake kuwafunga mdomo wakosoaji wao wakati walipotoka nyuma na kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Luton Town Jumapili.

**Luton walipata bao la mapema lililofungwa kwa kichwa na Elijah Adebayo, lakini Man City walipambana nakufunga mabao mawili kutoka kwa Bernardo Silva na Jack Grealish na sasa wamepitwa pointi nne na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool.**

"Hawahitaji kunithibitishia kile wanachoweza," alisema Guardiola katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Hili ni kundi la ajabu la wachezaji. Lakini ushindani na mahitaji ni kuthibitisha tena.

"Kwa ujumla, ni kawaida. 'Ndio, Jiji haliko sawa, Jiji limekwisha. 'Hiyo ni nzuri. Wacha wathibitishe kuwa wamekosea. Tunataka kushindana, nataka kuwa huko. Ni nzuri sana. Nilisema hapo awali, tunahitaji hiyo."

Matokeo hayo yalimaanisha City kumaliza rekodi ya kutoshinda mechi nne mfululizo ambayo ilitishia kuharibu msimu wao huku washindi hao mara tatu wakiwinda taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England.

> Niliwaambia tunapaswa kufanya nini, kujisikitikia? Hatupaswi kujihurumia...

Guardiola alifichua jinsi alivyoipa hamasa timu yake kwenye vyumba vya kubadilishia nguo wakati wa mapumziko.

"Niliwaambia tunapaswa kufanya nini? Kujisikitikia? Hatupaswi kujihurumia. Ni soka. Hii hutokea," alisema Guardiola.

"Sasa tunapaswa kufanya nini? Tucheze mchezo? Tujilalamikie? Washambuliaji tuwe wakali zaidi, tufunge mabao. Tulinde vema krosi dakika za mwisho na tuwe chanya. Tunapaswa kudai zaidi kutoka kwetu."

# CASEMIRO AIPA MATUMAINI MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imethibitisha kuwa kiungo wake, Casemiro amerejea mazoezini baada ya kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Kiungo huyo amekosa mechi nane hadi sasa kutokana na jeraha la misuli ya paja alilopata wakati wa kichapo cha mabao 3-0 kutoka Newcastle United kwenye Kombe la Carabao Novemba Mosi, mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa kwenye tovuti rasmi ya klabu, Man Utd ilitangaza kwamba hatimaye Casemiro amerejea mazoezini: “Casemiro ameanza mazoezi ya uwanjani, huku Mbrazil huyo akiongeza ahueni kwa Manchester United.”

Siku ya Jumapili, kiungo huyo alionekana akifanya mazoezi peke yake kwenye Uwanja wa Carrington.

Jeraha hilo la msuli wa paja lilikuwa la pili kuugua kwa mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid huku pia akiumia kifundo cha mguu alipokuwa akiichezea Brazil dhidi ya Venezuela.

Akiwa amekosa mechi tatu za klabu kutokana na jeraha la kifundo cha mguu, kiungo huyo alirejea uwanjani dhidi ya Newcastle, lakini akaambulia patupu tena wakati wa mapumziko kwenye mechi iliyopigwa Old Trafford.

Kurejea kwa Casemiro mazoezini, ingawa bado hajakichezea kikosi cha kwanza, ni habari njema kwa ‘Mashetani Wekundu’ na kunaweza kumaanisha kwamba Mbrazil huyo anaweza kurejea dimbani mapema kuliko ilivyotarajiwa.

Akizungumza mapema Novemba kuhusu ni lini alitarajia Casemiro na Lisandro Martinez kurejea dimbani, kocha Erik ten Hag alisema kwamba hakuwategemea wawili hao kurejea uwanjani kabla ya Krismasi.

# Pochettino alia na majeruhi Chelsea

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino ametoa taarifa za majeraha ya Reece James, Robert Sanchez na Marc Cucurella baada ya Chelsea kufungwa na Everton Jumapili.

Wachezaji wote watatu walilazimika kutolewa nje wakati wa kichapo cha mabao 2-0 katika Uwanja wa Goodison Park, huku nahodha James akitolewa kipindi cha kwanza kabla ya Sanchez na Cucurella kubadilishwa dakika kumi za mwisho za mchezo.

Majeraha hayo yanaongeza kwenye orodha ndefu ya wachezaji ambao hawajaicheza Blues.

Wesley Fofana, Romeo Lavia, Christopher Nkunku na Ben Chilwell ni miongoni mwa wachezaji wengine kumi wa kikosi cha kwanza ambao hawajacheza kwa sasa kutokana na majeraha.

“Reece alihisi kitu kwenye misuli yake ya paja. Hakika ameumia, lakini hatujui ni mbaya kiasi gani.

“Kwa kweli kwetu sisi ni mchezaji muhimu, mmoja wa mabeki bora wa pembeni duniani. Inasikitisha sana kwa sababu baada ya dakika 15 au 20 tulikuwa tunacheza vizuri na nadhani hali ya aina hii inatufanya tubadilike, kwa kweli. Malo Gusto anapata nafuu kutokana na jeraha lake.

“Hatukuwa tumetoa nafasi nyingi na unahitaji kuhamisha mambo ili kufanya mabadiliko. Hata Reece alipotoka nje timu ilikuwa ikisukuma na kucheza vizuri.

“Lakini tunasikitishwa kwa sababu unapoamini unaweza kujenga kitu na mchezaji kama yeye ambaye anafaa kuwa muhimu kwetu hawezi kuisaidia timu, tunarudi na kutathmini tena siku chache zijazo nini kinaendelea kwenye misuli yake ya paja. “



# *Son ataka Tottenham ishinde zaidi*

**LONDON,** England




HEUNG-Min Son aliitaka Tottenham Hotspur kuwa na mazoea ya kushinda baada ya ushindi mnono dhidi ya Newcastle United Jumapili.

Son mwenye umri wa miaka 31, alifurahi kurejea kwenye mstari wakati timu yake ikisonga mbele na kupitwa pointi tano na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool.

Aliiambia Sky Sports: “Unaposhinda unafurahia zaidi. Kurudi kama hivyo ni muhimu sana.

“Hatutaki kufanya makosa zaidi kama tulivyofanya. Nilidhani leo (juzi) ilikuwa nzuri.

“Natumaini tunaweza kuendelea kufanya hivi na kukaa wanyenyekevu.

“Tulisema tunapaswa kuwa wakorofi zaidi. Tulikuwa wakorofi leo (juzi) na tulikuwa tunatengeneza nafasi. Tulifanya kazi nzuri sana.

“Kushinda Newcastle 4-1 si rahisi. Ni timu yenye nguvu sana, kwa hivyo wapeni sifa wachezaji na mashabiki wote.

“Tunacheza Ligi Kuu, lazima tudaiane zaidi na zaidi.

“Haitoshi. Timu hizo za ajabu daima zinaendelea. Inapaswa kuwa tabia kwetu.

“Ikiwa tutaendelea kuwa na nguvu kama hii, tutakuwa upande mzuri sana.”

Ange Postecoglou alifurahishwa na jinsi timu yake ilivyocheza kwenye ncha zote za uwanja.

Aliongeza: Siwezi kuwakosea vijana. Wameweka juhudi kubwa leo (juzi).

“Tulikuwa waangalifu zaidi katika safu ya tatu ya mbele, nilidhani Son alikuwa bora na jambo kama hilo linawavutia watu wengine.”

HABARI MICHEZO

# SportPesa yazindua kampeni maalumu msimu wa Krismasi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI namba moja ya Michezo ya Kubashiri Tanzania, SportPesa, imezindua kampeni mahususi, ambayo inalenga kuwazawadia wateja wake zawadi mbalimbali ikiwamo fedha ijulikanayo kama 'KrismasiNaSportPesa'.

KrismasiNaSportPesa, inawapa nafasi wateja wa SportPesa kujishindia zawadi za pesa kila siku, wiki, bila kusahau kutakuwa na washindi kutoka mtaani kila wiki.

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano SportPesa, Sabrina Msuya, akielezea kampeni hiyo, alisema inatoa nafasi kwa kila mteja wa SportPesa kujishindia zawadi hata kama atakosa matokeo ya bashiri zake.

Alisema mteja akishajirekodi kupitia simu yake janja akielezea KrismasiNaSportpesa ina maana gani kwake msimu huu, ataipost video hiyo kisha anatakiwa 'kuwatag' marafiki zake 10, na kuwatumia DM numba yake ambayo amejisajili kwenye akaunti ya SportPesa na kwamba kila mshiriki ni lazima awe ameweka beti siku 14 zilizopita.

"KrismasiNaSportPesa" itadumu kwa muda wa siku 21, na kila siku watapatikana washindi wanne ambao watajishindia Sh. 100,000, pia kutakuwa na washindi wa wiki ambao watajishindia vocha ya Sh. 500,000 ili kufanya manunuzi kwa ajili ya Sikukuu ya Krismasi, na kila Alhamisi kutatolewa washindi wawili kutoka mtaani ambao hawa pia watajishindia vocha ya kufanya manunuzi ya Sh. 100,000.

"SportPesa inatoa rai kwa wateja wake wote kushiriki kampeni hii ili waweze kujizawadia zawadi hizi ambazo wataweza kufurahia msimu huu wa sikukuu na familia zao," alisema Sabrina.

Kampeni hii imeanza tangu Desemba 4 na itadumu hadi Desemba 22, mwaka huu.

"Ili kuweka bashiri yako na SportPesa tembelea tovuti yetu ya www.sportpesa.co.tz au piga *150*87# au wasiliana na huduma kwa wateja +255 764 115588," alihitimisha Sabrina.

# SIMBA, JKT QUEENS KUAMUA MFALME NGAO YA JAMII LEO

**Na Saada Akida**

SIKU iliyosubiriwa na wadau wa soka la wanawake kwa hamu kubwa kuona nani atakuwa bingwa wa kwanza katika Shindano la Ngao ya Jamii imewadia ambapo leo watajua ni JKT Queens ama Simba Queens, zitakapomenyana katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam kwenye mechi ya fainali kuwania taji hilo.

**JKT Queens ambao ni Mabingwa Watetezi wa Ligi ya Wanawake Tanzania, watakawakaribisha Simba Queens katika fainali ya kwanza ya mchuano huo.**

Mchezo huo wa fainali unatarajia kucheza saa 12:00 jioni, ukitanguliwa na mechi ya mshindi wa tatu kati ya Fountain Gate Princess dhidi ya Yanga Princess katika dimba hilo la Azam Complex majira ya saa 9:00 alasiri.

Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, alisema kubwa kwao wachezaji wana morali nzuri na wako tayari kwa ajili ya fainali hiyo kwa kukabiliana na wapinzani wao, Simba Queens.

Alisema maandalizi yako vizuri na baada ya fainali mechi ya robo fainali dhidi ya Fountain Gate Princess, walifanyia kazi mapungufu yao na ubora wa Simba Queens, hivyo mechi ya leo itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa kwa kuwa ni fainali.

"Hii itakuwa ni fainali na fainali haina dogo, tumewaona Simba katika mchezo wa nusu fainali dhidi ya Yanga Princess, lakini tunaenda kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunapata matokeo mazuri na kutwaa taji hili la Ngao ya Jamii," alisema Chabruma.

Kwa niaba ya wachezaji wa JKT Queens, Stumai Abdallah alisema kuelekea mechi ya leo wako tayari kisaikolojia na kimwili kuwavaa wapinzani wao, Simba Queens.

Kocha Msaidizi wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema wanaelekea mwanzoni mwa msimu na ikumbuke mechi ya msimu uliopita walipoteza dhidi ya JKT Queens na kushindwa kufikia malengo yao.

Alisema utakuwa mchezo mgumu kwa sababu wanahitaji kulipa kisasi cha kuhakikisha wanafanikiwa kupata matokeo mazuri na kwamba waliona ubora wa JKT Queens hivyo watacheza kwa tahadhari kubwa ili kufikia malengo yao.

"Hii ni fainali mbili, moja ni kutaka Ngao ya Jamii, lakini pia Simba kufuta ufalme wa JKT Queens ambao walikuwa nao kwa msimu uliopita," alisema Mgosi.

Aliongeza kuwa wamejipanga vizuri na wanatarajia kuona ushindani mkubwa kwa sababu msimu huu wamejipanga kuhakikisha wanafanikiwa kurejesha heshima ya Simba kwa kuanza kutwaa taji hilo la Ngao ya Jamii kwa mara ya kwanza.

Naye Mchezaji wa Simba, Vivian Corazon, alisema wamefanya maandalizi mazuri na mpira ni dakika 90, hivyo wamejipanga vizuri kushindana vya kutosha dhidi ya JKT Queens.

"Tunaenda kushindana ipasavyo kuhakikisha tunafanya vizuri na kutwaa ubingwa, sawa tunajuana, lakini tunaweka pembeni kujuana na kupambana dakika 90 kutafuta ushindi," alisema Corazon.




Wachezaji wa mchezo wa kuogelea wakishindana katika mashindano ya Justfit Inter Schools Games, yaliyofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga SC, Chivaviro sasa kimeeleweka*

INATOKA UKURASA 24

"Kwa sasa hatua mshambuliaji mzoefu halisia na Kocha Gamondi amewataka viongozi kuanza na jambo hilo na tayari Hersi alifanya kikao na viongozi wa Kaizer Chiefs kwa ajili ya kumalizana na Chivaviro.

"Kikao hicho kimeenda vizuri na sasa imebaki hatua chache, ila haijafahamika vizuri ukubwa wa mkataba wake aliomalizana na Yanga na muda atakaojiunga nao kambini, ila taarifa za uhakika ni kwamba Chivaviro atakuwa miongoni mwa nyota atakayecheza Yanga," alisema.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari na Mawasiliano wa Yanga, Ally Kamwe, zoezi la usajili wa dirisha dogo wameshakamilisha na sasa wanasubiri kazi ya kutambulisha.

Alisema Kocha Gamondi tayari amekabidhi ripoti na tayari imeshafanyiwa kazi kwa kusajili mchezaji ambaye atakuja kuwa msaada kwenye timu ikiwamo safu yao ya ushambuliaji ambayo imefanyiwa kazi.

"Ni kweli tutafanya usajili kulingana na mapendekezo ambayo ameyaomba Gamondi, tayari kazi imefanyika, kwa rais wetu, Hersi kufanya kazi ya usajili mapema sana na tutashusha mtu hatari ambaye atakuja kukata kiu cha mashabiki wetu," alisema Kamwe.

# Benchikha abakiza kazi

INATOKA UKURASA 24

kuwa tutakuwa nyumbani kama ilivyokuwa kwao," ameongea kocha huyo.

Benchikha alilalamikia kitendo cha mwamuzi wa mechi hiyo kuongeza dakika tatu baada ya tatu za majeruhi kumalizika.


"Aliongeza dakika tatu tukacheza hadi dakika ya 96, si kitu cha kawaida sijui kwa nini alifanya hivyo, lakini ndio hivyo," alilalamika Benchikha.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, hakusita kumpa sifa kocha huyo akisema ni mwanamapinduzi aliyefanya mapinduzi makubwa ndani ya kikosi hicho kwa muda mfupi tu.


"Ndani ya muda mfupi amefanya mapinduzi makubwa ndani ya kikosi chetu, utimamu wa mwili kwa wachezaji umepanda maradufu, ukabaji wa hali ya juu, ufundi umeongezeka kwa baadhi ya wachezaji wetu, kiwango cha mchezaji mmoja mmoja kimepanda, hali ya kujiamini imeongezeka na morali iko juu," alisema.

Simba imerejea nchini jana alfajiri na wachezaji kupewa mapumziko ya siku moja kabla ya leo kuanza mazoezi kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar na kisha Jumanne ijayo kuikaribisha Wydad katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Michezo
Jumanne Desemba 12, 2023
Nipashe



Casemiro aipa matumaini United UKURASA 22




Ranga Chivaviro

# Yanga, Chivaviro sasa kimeeleweka

**Na Saada Akida**

●●● Uongozi wasema tayari kazi imefanyika na wamemaliza usajili mapema, kilichobaki...

ZIKIWA zimebaki takriban siku tatu kabla ya dirisha dogo la usajili Tanzania Bara kufunguliwa, mabosi wa Klabu ya Yanga wamefikia hatua nzuri ya mazungumzo na uongozi wa Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini juu ya uwezekano wa kuinasa saini ya mshambuliaji wa timu hiyo, Ranga Chivaviro, imefahamika.

**Yanga imekuwa ikitafuta mbadala wa Fiston Mayele aliyetimkia Misri katika Klabu ya Pyramid ambapo nafasi yake ilitarajiwa kuzibwa na Hafiz Konkoni, ambaye hata hivyo ameshindwa kuonesha makali yake ndani ya kikosi hicho hali iliyosababisha klabu hiyo kuelekeza nguvu zao katika kuisaka saini ya Chivaviro mwenye umri wa miaka 31.**

Hata hivyo, licha ya uongozi wa juu wa klabu hiyo kuweka bayana kuwa suala la usajili ndani ya timu hiyo kwa sasa lipo chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, lakini Nipashe limefahamishwa kwamba tayari mabosi wa timu hiyo wamekuwa na mawasiliano mazuri na viongozi wa Kaizer Chiefs juu ya uwezekano wa kumnunua mshambuliaji huyo ama kumpata kwa mkopo.

Chanzo cha kuaminika kutoka ndani ya klabu hiyo kimeliambia Nipashe kuwa kwa sasa wapo katika mazungumzo ya kuona wanalimaza vipi na kumpata mshambuliaji huyo wa kati raia wa Afrika Kusini.

"Ni kweli tumekuwa na mazungumzo na viongozi wa timu ambayo anacheza huyo mchezaji kwa sababu bado nafasi ya mshambuliaji wa kati imekuwa tatizo na huyo mtu tunaona anaweza kutusaidia katika eneo ambalo tumeshindwa kupata dawa, kama kila kitu kikienda sawa basi tunategemea kuwa naye hapa," alisema mtoa taarifa wetu.

Mtoa habari huyo alisema baada ya kufikia mapendekezo hayo, viongozi kupitia rais wa klabu hiyo, Hersi Said, alikuwapo Afrika Kusini kuzungumza na Kaizer Chiefs kwa ajili ya kuinasa saini ya nyota huyo.

INAENDELEA UKURASA 23

# Benchikha abakiza kazi moja tu Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amekiri kuwa kikosi chake kinazidi kuimarika ila kuna tatizo moja la ufungaji ambalo ameahidi kulifanyia kazi, akisifu kiwango cha wachezaji wake, lakini akilia na mwamuzi aliyechezesha mechi ya raundi ya tatu ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca Jumamosi iliyopita, akisema aliongeza dakika tatu zaidi kitu ambacho si cha kawaida.

Akizungumza jana baada ya kuwasili nchini akitokea, Morocco ulipochezwa mchezo huo katika Uwanja wa Marrakech na Simba kufungwa bao 1-0 lililowekwa wavuni dakika za majeruhi, Banchikha alisema mechi ilikuwa nzuri ingawa ilikuwa na baadhi ya changamoto zilizosababisha wakose matokeo mazuri.

"Tulicheza vizuri, tuliwafanyia Wydad 'pressing' hadi dakika ya 90, tukafungwa goli dakika za mwisho ambalo ni kama tulikosa umakini hadi mwisho wa mchezo.

"Ninachofurahia kwenye timu yangu ni kuweza kuzuia na kushambulia kwa kasi, eneo la kuweka mpira nyavuni ndilo tumeshindwa kufanikisha, nadhani kuna haja ya kukaa na kulifanyia kazi, lakini nimeridhishwa na timu ilivyocheza," alisema kocha huyo raia wa Algeria ambaye hana muda mrefu tangu aitwae timu hiyo kutoka kwa Mbrazili Robertinho Oliveira.

Alisema kwa sasa wamerejea nyumbani kujiandaa na mechi ya marudiano ambayo atataka kujipanga vizuri kuhakikisha Simba inaibuka na ushindi.

"Mechi ya marudiano tutajipanga vizuri na kuhakikisha tunakuwa sahihi zaidi ili nasi tushinde kwa

INAENDELEA UKURASA 23



Mshambuliaji wa Simba, Jean Baleke akiwa kazini dhidi ya Wydad Jumamosi iliyopita nchini Morocco.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002